epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Mei 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581672
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

## KLABU MBILI ZAMTAKA GREENWOOD

# Mambo 8 kupaisha sekta maji 2024/25

UKURASA 2




Illustration: Kondo Haruni Kondo, binharun79@gmail.com

"Serikali itaendelea kutekeleza miradi 1,095 ya usambazaji maji vijijini katika maeneo mbalimbali nchini na kuchimba visima vitano kwenye kila jimbo la uchaguzi maeneo ya vijijini ikianza na visima 900. Hali hiyo itaongeza upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa asilimia 79.6 hadi zaidi ya 85 ifikapo mwaka 2025.

**Waziri wa Maji, Jumaa Aweso**

UKURASA WA 4

## ACT WAZALENDO YAKEMEA KURA FEKI UCHAGUZI

CHAMA cha ACT Wazalendo kimekemea matumizi ya kura feki katika uchaguzi wa serikali...

UKURASA WA 4

## SABABU IDADI NDOGO MATIBABU WATOTO KIFAFA BAYANA

TAASISI ya Wazazi wa Watoto Wanaoishi na Kifafa, imezindua kampeni ya kuhamasisha jamii...

UKURASA WA 8

## MWALIMU MBARONI TUHUMA KUMBAKA MWANAFUNZI WAKE

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Katoro (jina linahifadhiwa) miaka 36 anadaiwa kumbaka...

## Samia aagiza kulegezwa masharti uwekezaji

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa ndani ya gari lililounganishwa katika Kiwanda cha Kuunganisha Malori na Matipa cha Saturn Corporation Ltd, baada ya kuzindua kiwanda hicho, Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Utata waibuka sakata nyumba milioni 50/- kuuzwa kwa milioni 3/-

UKURASA 3

MICHEZO MILIONI 300/- ZAMBAKISHA KIBU SIMBA UK.24 KATUNI UK.6

# Samia aagiza kulegezwa masharti uwekezaji

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kupunguza urasimu na kulegeza masharti ili kuvutia uwekezaji.

Amesema hatua hiyo itachochea uwekezaji na viwanda kujengwa kwa wingi, hivyo kuongeza ajira na mapato serikalini.

Pia amesema ili kuchochea ukuaji wa viwanda, serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, itajielekeza kuwezesha kuzalisha viwanda vinavyosaidia vingine na kwamba katika kutekeleza sera ya viwanda, kuna haja waziri kuhakikisha viwanda vinasomana.

Akizungumza jana Kigamboni, Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kuunganisha magari makubwa ya Howo kinachomilikiwa na kampuni ya Saturn Corparation Limited, alisema amekuwa akizungumzia suala la mifumo kusomana ili kurahisisha ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya uwekezaji na viwanda.

"Viwanda vitambuane na visomane, nani anamzalishia nini nani, ili tutengeneze 'block chain'. Lakini pia ni fursa ya kuwa na kongani za viwanda vidogo vingi vitakavyolisha vikubwa ili vizalishe kwa haraka na kwa bei nafuu na tuingie kwenye soko tukiwa washindani wakubwa," alisema.

Rais Samia alizielekeza wizara hizo kumaliza haraka suala la mgodi wa Mchuchuma na Liganga ili kupata kampuni nzuri itakayoanza kuchimba chuma ili kitumike kama malighafi katika kiwanda hicho na vingine vitakavyokuwa na uhitaji.

Alisema serikali imeimarisha mazingira ya uwekezaji ikiwamo kupunguza kodi ya kampuni kutoka asilimia 30 hadi 10 kwa kipindi cha miaka mitano ili kuchochea uwekezaji, ajira, na kurahisisha upatikananji wa magari.

Pia alibainisha kuwa anafarijika baada ya kuona kiwanda hicho kimeshatoa ajira za moja kwa moja 250 na zisizo za moja kwa moja takribani 1,800 na kwamba hiyo ni hatua nzuri itakayoongeza mzunguko wa fedha.

"Uamuzi wa kampuni hii utachangia ukuaji wa sekta zingine kama kilimo, madini na usafirishaji kwa kuongeza uwezo na ufanisi wa shughuli za uzalishaji. Pia kiwanda hiki kitatumia vioo vinavyozalishwa na kiwanda kingine ambacho zaidi ya asilimia 80 ya malighafi zinapatikana nchini," alisema.

Rais Samia alisema baada ya kuangalia kiwanda hicho, amebaini kuna vitu vingi vinaweza kuzalishwa hapo na kwamba anaendelea kuwavutia wawekezaji kuja kuweka viwanda vingine nchini, huku akimwelekeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, kuhakikisha mnyororo huo haukatiki.

Pia alisema amejulishwa kwamba idadi ya vipuri vinavyotumika kuunganisha gari moja katika kiwanda hicho ni takribani 2,400 ambavyo vingi vinatoka nje na kuweka bayana kuwa hiyo si afya kwa ukuaji wa viwanda na anaiona kama fursa kwa Watanzania.

Alisema wanaweza kunufaika zaidi kupitia uwekezaji wa viwanda vingine vya uzalishaji wa vipuri vya magari na mitambo na kwamba kuna malighafi zinazopatikana nchini kikiwamo chuma kilichoko Mchuchuma na Liganga ambacho kinaweza kutumiwa na kiwanda hicho.

Rais alisema jitihada za kuvutia mitaji na uwekezaji nchini ni jambo la kuungwa mkono na kila mmoja na kila mdau ana wajibu wa kuhakikisha uwekezaji unadumu na unakuwa endelevu.

Serikali kwa upande wake, alisema ina wajibu wa kuendelea kuimarisha mazingira bora na yanayotabirika kufanyia biashara.

Alisema wawekezaji wana wajibu wa kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuwa na bei shindani ndani na nje. Pia alisema wananchi wana wajibu wa kujifunza haraka teknolojia inayoletwa na wawekezaji, kufanya kazi kwa bidii na kwa uaminifu.

Waziri wa Viwanda na Biashara Dk. Ashatu, alipongeza viongozi na menejimenti ya kiwanda hicho kwa kuwaamini na kuamua kuwekeza nchini, huku akiwatoa wasiwasi kwamba wako pamoja na watashirikiana kila hatua.

Alisema viwanda na biashara ndio msingi wa uchumi wa taifa na kwamba uwekezaji ambao uko juu kwa sasa nchini ni sekta ya viwanda na biashara na ndizo zilizoajiri Watanzania wengi kuliko sekta zingine.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Rwelu, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, wakivuka barabara iliyojaa maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, wakati wakienda shuleni jana. **PICHA: HAMISI NASRI**


**INVITATION FOR BIDS**
**FOR**
**SALE OF ASSETS LOCATED AT PLOT NO. 129 & 130 BLOCK 216 KIPAWA INDUSTRIAL AREA, ILALA DAR ES SALAAM.**

1. Notice
Notice is HEREBY GIVEN THAT under power contained in the Debenture Deed dated 24th September 2010 and First Deed of Variation of Debenture dated 16th August 2012, Second Deed of variation of Debenture dated 8th May 2014 and Third Deed of variation of Debenture dated 3rd April 2017 respectively and between PRINCE AFRICA LIMITED OF P.O Box 5838 Dar es Salaam (Borrower) and I & M Bank (T) Limited and every other power enabling me so to do, I Annette W. Kirethi being the Receiver/Manager of the entire charged assets, in Receivership hereby place the Borrower's assets for sale by way of tender.

2. Bidders are invited for the purchase of the following assets; pipe threading machine, spanner too kits (various sizes), metallic beds, wire binders, filter machine, water tanks (simtank), lathe machine, bench grinder, bench drill machine, hoppus, communication towers, isolators(switch gears), water purification machine, gas cylinders, jig saw, office tables, office chairs, computer, land line phones, office cupboards (small and big), metallic shelves, standing fans, flat screen monitors, printers, UPS machines, CPUs, plastic chairs (small and big), fire extinguishers, plastic containers (small and big), plastic jugs (small and big), office cupboards, small weighing scale, basins (small and big), used desktop computers, metallic ladders (small and big), Motor vehicles: Toyota (Porte) and (Cresta).

A full list shall be made available upon request.

3. All the assets are located at Plot No. 129 & 130 Block 216, Kipawa Industrial Area, Ilala Dar es Salaam.

4. Viewing dates for all bidders shall be conducted on 10th May, 2024 and 11th May, 2024 between 14:00hrs-16:00hrs.

5. Each Tender document should be submitted in sealed envelopes with the specific lot number on the outside indicating;

(i) The identification of the assets specific item and quantity proposed to be purchased
(ii) The offer price for each asset bid for
(iii)Full address and contact details of the bidder including contact telephone number and email address where possible. The bidder must inspect the assets and offer a price to purchase on the basis of that inspection only

6. The Assets shall be sold strictly on 'as is where is' basis.

7. The Purchased assets shall be removed from the site within two (2) days from date of full payment of the purchase price at bidder's cost. Thereafter, there shall be a storage fee charged for each additional day of storage.

8. The Receiver/Manager is not bound to accept the highest bid or any bid at all.

9. The Receiver/Manager does not provide any warranty as to the condition of the equipment and machinery. Bidders are advised to inspect the equipment and seek professional opinion on the respective condition.

10. Any photograph and or description of the assets supplied herein are without liability of the Receiver/Manager as to their correctness. Independent valuation is strongly recommended.

11. The successful bidder shall be bound to pay 60% of the agreed purchase purchase price within 48 hours of being declared successful and without deduction within 3 days from date of notification.

12. Should the successful bidder or intended purchaser fail to meet any of the terms of sale including but not limited to failure to pay the purchase price as provided above, the sale of such assets shall be cancelled and 10% of the bid amount a shall be forfeited.

13. Deadline:
Bids shall be submitted so as to reach the Receiver/Manager on the address below on or before Wednesday 15th May 2024 at 16:00 hours. Bids shall be opened at 16:30 hours thereafter at the Receiver/Manager's Offices. Successful bidders shall be notified within five days from the date of opening.

**BID ADDRESS**
**Annette W. Kirethi**
**Receiver/Manager - Assets of Prince Africa Limited**
**C/O Hallmark Legal**
**18 Chole/Ruvu**
**Masaki Area**
**P.O. Box 13811**
**Dar es Salaam**
**Tel: 0715260035 / 0762752746**
**Email: info@hallmarkattorneys.co.tz;**

**LATE SUBMISSIONS WILL BE DISREGARDED**


# Mambo 8 kuipaisha sekta ya maji 2024/25

**Na Jenifer Gilla**

WIZARA ya Maji imeanika vipaumbele vinane kwa mwaka 2024/25 vinavyolenga kuboresha huduma ya maji kwa kusambaza majisafi na salama kwa zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wa vijijini na zaidi ya asilimia 95 wa mijini.

Katika kufikia malengo hayo, serikali kupitia Wizara ya Maji, imesema itaongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na uendeshaji wa skimu za maji.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/25 Waziri wa wizara hiyo, Jumaa Aweso, aliomba Bunge kupitisha Sh. bilioni 627.78 ili kutekeleza vipaumbele hivyo ambavyo vitazingatia kuimarisha usimamizi, uendelezaji, uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na kuimarisha na kusimamia huduma za ubora wa maji.

Alitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kukamilisha utekelezaji wa miradi inayoendelea na kuendelea na ujenzi wa miradi mikubwa, kuongeza kasi ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati na ya kimkakati, kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji ambavyo havina huduma, kukamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji, Mtandao wa Taifa wa Kusambaza Maji na mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji.

"Kipaumbele kingine ni kukamilisha na kupunguza upotevu wa maji, kuongeza kasi ya ufungaji wa dira za malipo kabla ya matumizi ya maji, kuongeza kasi ya uwekezaji kwenye usafi wa mazingira na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na uendeshaji wa skimu za maji," alisema Aweso.

Alisema katika mwaka ujao wa fedha, serikali itakarabati miradi ya maji na kudhibiti wizi wa maji ili kupunguza kiwango cha maji yanayopotea kutoka wastani wa asilimia 35.3 ya maji yanayozalishwa hadi kiwango kinachokubalika kimataifa cha asilimia 20.

Hali hiyo pia alisema inahusisha ukarabati wa miundombinu ya maji iliyochakaa, kufunga dira za maji ya jumla na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji.

Alisema itaendelea kufanya tathmini na ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji 2,200, mifumo ya usambazaji maji 8,245 vijijini na mijini na mifumo 150 ya majitaka.

Pia alisema serikali imepanga kuweka mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu na taarifa za ubora wa maji; kuendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza madini ya flouride kwenye maji ya kunywa na ya kupikia na kuwezesha uandaaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya usalama wa maji katika mamlaka za maji 40 na CBWSOs 120.

Waziri Aweso alisema serikali itaendelea kuimarisha mfumo wa kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji ikiwamo ukarabati wa vituo 100 vya usimamizi wa rasilimali za maji, kutoa vibali 600 vya matumizi ya maji, kuunda jumuiya 18 za watumia maji na kuunda kamati tisa za vidakio vya maji.

Alisema wizara pia itaimarisha uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kutambua vyanzo vya maji juu ya ardhi na maeneo yenye hifadhi ya maji chini ya ardhi. Na kufanya utafiti wa kina ardhini ili kutambua maeneo yenye maji na kuyafanya kuwa maeneo tengefu ili kuhakikisha usalama wa maji unakuwapo.

"Serikali itaendelea kutekeleza miradi 1,095 ya usambazaji maji vijijini katika maeneo mbalimbali nchini na kuchimba visima vitano katika kila jimbo la uchaguzi kwenye maeneo ya vijijini ikianza visima 900. Hali hiyo itaongeza upatikanaji huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa asilimia 79.6 hadi zaidi 85 ifikapo mwaka 2025," alisema.

Pia alisema serikali itaendelea kubadili mitambo inayotumia dizeli na kuweka umeme wa gridi ya taifa au nishati ya jua ili kupunguza gharama za uendeshaji wa skimu za maji na kuimarisha usimamizi wa mauzo ya maji na makusanyo kwenye CBWSOs kwa kufunga mfumo wa malipo kabla ya matumizi, kuweka mfumo wa pamoja wa ankara za maji na kujiunga kwenye mfumo wa makusanyo ya fedha za umma.

"Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo pamoja na sekta binafsi imepanga kutekeleza jumla ya miradi 247 ya maji mijini. Lengo ni kuhakikisha zaidi ya asilimia 95 ya wakazi wa mijini wanapata huduma ya majisafi na salama ifikapo mwaka 2025," alisema Aweso.

HABARI KITAIFA

## Serikali kusaidia wachimbaji wadogo

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, ameainisha mpango wa serikali wa kusaidia utatuzi wa changamoto zinazowakabili wachimbaji wadogo nchini.

Waziri Mavunde aliyasema hayo jana, wakati akijibu swali la Dk. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum aliyetaka kujua mpango wa serikali kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini Wilaya ya Ulanga.

Alisema, mpango wa serikali ni kuwasaidia wachimbaji wadogo nchini wakiwamo wa madini wa Wilaya ya Ulanga unaohusisha masuala mbalimbali ikiwamo kuwekeza zaidi katika utafiti wa kina kugundua madini katika maeneo mbalimbali ili kuwaongoza vizuri wachimbaji wadogo.



"Spika maeneo mengine ni utoaji wa leseni za uchimbaji kwa wachimbaji wadogo; kutoa elimu ya matumzi ya teknolojia sahihi ya uchimbaji ili kuongeza tija; huduma ya uchorongaji kwa gharama nafuu kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)," alisema Waziri Mavunde.

Vilevile, alisema mpango mwingine ni kuwezesha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wachimbaji; na fursa ya ukodishaji wa mitambo na vifaa chini ya usimamizi wa STAMICO.

# Utata waibuka sakata nyumba mil. 50/- kuuzwa kwa mil. 3/-

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

SAKATA la nyumba yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50 kuuzwa kwa Sh. milioni tatu kufidia deni la chama cha akiba cha kuweka na kukopa (SACCOS) limezidi kuchukua sura mpya.

Hatua hiyo ni baada ya nyaraka za vitabu vya usharika kuonyesha iliuzwa kwa Sh. milioni saba huku ikidaiwa iliuzwa kwa Sh. milioni 45.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Usharika Mkoa wa Arusha, Grace Masambaji, alisema wana taarifa kuwa Kalista Nassoro alikopa Sh. milioni tatu kutoka SACCOS ya Kijenge lakini akawa anasuasua kurejesha mkopo huo.

"Muda wa marejesho uliisha akaanza kurejesha baada ya kupatiwa barua kutoka kwenye kamati ya usimamizi ya mikopo. Alirejesha kidogo baadaye wakaona bado anaendelea kusumbua.

"Walichokifanya ambalo ni kosa kubwa kutoka kwa viongozi wa bodi, walichukua kampuni ambayo haina kibali kutoka Tume ya Maendeleo ya Usharika Tanzania ambayo ni Mangwembe,"alisema.

Masambaji alisema pia ofisi ya usharika haikushirikishwa wala mrajis na kwenda kuuza nyumba hiyo bila kumshirikisha Nassoro, jambo ambalo alisema halikuwa sahihi.

"Mhusika wakati anarudi alikuta vitu vyake vya nyumba vyote vimetolewa nje na habari ambazo sina uhakika, inasemekana hiyo nyumba iliuzwa kwa Sh. milioni 45. Inasemekana thamani ya hiyo nyumba ni kama Sh. milioni 50 maana ina vyumba saba vya wapangaji na iko katika eneo nzuri," alisema.

Aidha, alisema kinachosomekana katika vitabu vya chama imeuzwa kwa Sh. milioni saba "Hapo kuna utofuati kati ya Sh.milioni saba na Sh. milioni tatu hata hiyo Sh. milioni nne iliyobaki hawakumpatia ni wizi mkubwa ulifanyika."

Alisema kampuni ya udalali ya Mangwembe iliyouza nyumba hiyo, imekuwa ikilalamikiwa kufanya ubadhirifu wa mali za wananchi.

"Hapa kuna chama cha usharika kimekuja leo (jana). Mwaka 2017 walimpa tenda Mangwembe ya kukamata magari ya wanachama wawili. Hajaleta hela kwenye chama na ameuza hayo magari hela haijaletwa.

"Inasemekana gari moja lilionekana kwenye kampeni wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro baadaye likaja kukamatwa na polisi, likaachiwa na halijaonekana mpaka leo. Ni magari makubwa tu, mmoja alikuwa anadaiwa Sh. milioni 37 na mwingine alikuwa anadaiwa Sh. milioni saba," alisema.

Aidha, alisema tatizo kubwa lililopo kwa mkoa wa Arusha, wananchi wanachukua mikopo na hawataki kurejesha na kwamba wakiguswa wanakimbilia mahakamani na kesi hizo ziko nyingi.

Masambaji alisema mtu anapochukua mkopo kwenye vyama vya usharika ni muhimu akalipa kwa wakati.




Vigezo na Masharti Kuzingatiwa

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian




Kituo cha kisasa cha mabasi Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam kikionekana kusuasua licha ya kukamilika kwa ujenzi wake uliogharimu mabilioni ya fedha za mapato ya ndani ya manispaa hiyo, kama ilivyonaswa na kamera yetu jana, ambapo abiria walionekana kukaa muda mrefu bila kupata huduma ya usafiri. **PICHA: JOHN BADI**

# ACT yakemea kura feki katika uchaguzi

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimekemea matumizi ya kura feki katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ambazo kimesema zinawanyima wananchi haki ya kupata viongozi wanaowataka kwa ajili ya maendeleo ya maeneo yao.

Aidha, kimependekeza kuwapo kwa uwazi na ushirikishwaji katika uzalishaji, utunzaji na usambazaji wa karatasi za kupigia kura ili kudhibiti kura feki kwenye uchaguzi huo.

Mwenyekiti wa Chama hicho taifa ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, alisema hayo jana wakati akizungumza na wazee wa chama hicho mkoani Kigoma.

Wazee hao walimweleza kusikitishwa na kushamiri kwa matumizi ya kura feki katika uchaguzi, wakiituhumu tume hiyo na vyombo vingine vya serikali kuhusika ili kukipa ushindi chama tawala.

Othman alisema anafahamu hujuma zinazofanyika katika uchaguzi ikiwemo matumizi ya kura feki na kuwasihi wanaofanya vitendo hivyo kuacha kwani chama hicho kitaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuzikomesha.

Alisema chama hicho kinapendekeza wajumbe waliopo wajiuzulu ili wapya wapatikane kwa utaratibu uliowekwa kwenye sheria pia kuwapo kwa uwazi na ushirikishwaji katika uzalishaji, utunzaji na usambazaji wa karatasi za kupigia kura ili kudhibiti kura feki kwenye uchaguzi.

"Tatizo letu halijawahi kuwa jina la tume, tatizo letu ni muundo ambao unaifanya tume isiwe huru. Mabadiliko ya muundo wa Tume ya Uchaguzi yanapaswa kwenda sambamba na mabadiliko ya wajumbe wa tume hiyo.

"Wajumbe wa sasa kuendelea ni sawa na mtu yuleyule anajiita kuwa ni mtu mwingine kwa sababu tu amevaa nguo tofauti," alisema.

Othman pia alikutana na kuzungumza na Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Kigoma, Joseph Mlola, na kuwapongeza viongozi wa dini kwa mchango wao katika kuliombea na kuliunganisha taifa.

Pia alimshukuru Askofu huyo kwa kukipongeza chama hicho kutimiza miaka 10 na kumhakikishia kuwa rai yake kwa chama ya kuwa sauti ya wasio na sauti itazingatiwa.

Alimweleza Askofu Mlola kuwa uamuzi wa Halmashauri Kuu ya ACT Wazalendo kujitoa kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na kuwa wameshawaandikia barua Rais

Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali mwinyi wa Zanzibar.

"Mpira uko kwao kufanyia kazi masuala ambayo ACT Wazalendo imeyasisitiza hasa mageuzi katika mfumo wa uchaguzi na haki Zanzibar kwa sababu iwapo masuala hayo yasipofanyiwa kazi, ACT Wazalendo itatekeleza uamuzi wake wa kujitoa," alisema.

# Sababu idadi ndogo matibabu watoto kifafa zaanikwa

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Wazazi wa Watoto Wanaoishi na Kifafa, imezindua kampeni ya kuhamasisha jamii kuhusu uelewa wa maradhi hayo na kueleza kuwa, idadi kubwa ya waliokuwa wakihudhuria kliniki imepungua kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo suala la bima.

Daktari Bingwa Mbobezi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Said Kuganda, ambaye ni Mwenyekiti wa taasisi hiyo ambayo pia, inalenga wanaoishi na hali ya kifafa, aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo hospitalini hapo.

Bingwa huyo alisema: "Zamani tulikuwa na mfuko wetu maalum tunatafuta wafadhili wanatuongezea fedha kisha tunatafuta dawa kiasi, hivyo aliyekuwa akikwama tulikuwa tunampatia dawa.

"Ilipokuja bima ya afya, watoto wengi walijiunga huko. Kwa hiyo dawa za kawaida zikawa zinapatikana huko. Kasi ya mfuko wetu ikapungua kwa kuwa, wengi walijiunga katika bima ya afya, wakawa wanapata huduma hata kwa watu wazima.

"Bahati mbaya bima ya watoto ikafutwa ili kuanzisha iliyo bora zaidi. Tangu ifutwe na inayoboreshwa bado haijaja, tumerudi kwenye changamoto, wazazi wengi wanalalamika, hawaji tena kwenye kliniki kwa kuwa, kila wakija wanaambiwa wanunue dawa, bima haifanyi kazi tena.

"Tumebaki na hii changamoto ambayo kidogo tunasema tuongeze sauti ifike kwa jamii kujaribu kuangalia namna wanavyoweza kusaidia jambo hili.

"Tunajua serikali inafanya vizuri, lakini kama wananchi tufanye juhudi kujulisha serikali kwamba, kuna watu wenye hizi hali hawana bima, hivyo imekuwa shida na wanapungua katika kliniki zetu."

Alisema mtazamo wao bado .

anaitegemea serikali na wanaamini wataboresha huduma ikiwamo wenye kifafa.

"Tunaamini kitakachokuja kitakuwa kizuri zaidi, lakini tunataka serikali ijue kuna watu wanashindwa kuja kupata huduma kwa sababu ya hizi changamoto," alisema.

Hata hivyo, mtaalum huyo alishukuru serikali kwa kuwa kwa mwaka huu, baadhi ya dawa nzuri mpya zimeanza kuingizwa katika kifurushi cha bima, lakini changamoto iliyoko ni watu hawana kifurushi chenyewe.

"Watoto wengi wanachukua bima shuleni, kwa hiyo kwa watoto wa kifafa wanaougua sana huwa hawaendi shuleni. Na asipokwenda anajikuta hapati huduma. Tunaposema kuondoa unyanyapaa ni kujaribu kusaidia katika haki zao za msingi," alisema.

Alisema wanaomba serikali iangalie kwa kuwa wazazi wameshachoka na watoto wao wanahitaji tiba.

"Wengi wamepungua na hatuwezi kusema kwa namba. Sababu zipo nyingi hii ni kutokana na swali, lakini nyingine ni unyanyapaa ambao kabla hawajapata tiba nzuri unakuta mganga wa kienyeji ameshamwambia (mzazi au mlezi) tiba iko huku.

"Kwa sasa ukitembelea Ifakara, mkoani Morogoro kwa sababu ya visababishi vipo vingi imegundulika watu wengi pale wameathirika tatizo la kifafa, wapo kwenye matibabu na utafiti unaendelea, lakini inaonyesha kuna utofauti na maeneo mengine.

"Ila kila maeneo Tanzania kuna watu wanaishi na hali ya kifafa. Mfano hapa (Tanzania) wanasema karibu katika watu 1,000 kati ya 20 mpaka 37 huwa na hiyo hali, lakini kwenye huyo maeneo ambayo hali hii inaonekana ni kubwa zaidi," alisema.

Alisema wamekuwa wakihamasisha wenye kifafa kuwa makini na kufuatilia dawa na matibabu kwa ujumla kwa kuwa, tiba sahihi ikifuatiliwa mara nyingi matukio kama hayo hupungua.

Kuhusu kampeni waliyozindua, mtalaam huyo alisema, itafanyika kwa mwaka mzima na ifikapo mwezi Novemba, mwaka huu, watakuwa na mdahalo wa kitaifa kuhusu kifafa na namna bora ya kuwasaidia wanaoishi na hali ya kifafa.

Mgonjwa anayeishi na kifafa, Dk. Mary Kipingili, alisema kaulimbiu ya kampeni hiyo inasema, "Elimika juu ya kifafa, tokomeza unyanyapaa, pata tiba sahihi."

Aliishukuru serikali kwa kutoa kipaumbele na kuboresha afya za wananchi wake, hasa katika kuzuia na kutibu magonjwa yasiyoambukizwa, kifafa kikiwa ni miongoni mwa maradhi hayo yanayotokana na hitilafu katika mfumo wa umeme wa ubongo.

Alisema kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), takribani watu milioni 50 wanasumbuliwa na hali za kifafa, huku katika Bara la Afrika kukiwa na zaidi ya watu milioni 10 wanaishi na hali hiyo.

"Inakadiriwa kuwa watu milioni sita hubainika na hali hii kila mwaka. Hapa Tanzania zaidi ya watu milioni moja huishi na hali za kifafa.

"Kwa bahati mbaya kabisa uelewa wa wanajamii kuhusu hali hizi za kifafa bado ni mdogo, hivyo kumekuwapo na vitendo vya unyanyapaa na kubaguliwa kwa watu wanaoishi na hali za kifafa," alisema.

Mary alisema unyanyapaa na kubaguliwa imechangia wao kukosa haki zao za msingi katika maisha yao ya kila siku na hivyo kudhoofisha ubora wa maisha yao. "Kumekuwa na visa mbalimbali vya kufukuzwa shule au kutopelekwa shule kabisa, kutoajiriwa au kufukuzwa kazi, kuvunjika kwa mahusiano au ndoa unapogundulika kuwa na hali za kifafa, na hata kufanyiwa vitendo vya kikatili vinavyotokana na imani za kishirikina," alibainisha.

Aidha, alisema vitendo hivyo huleta msongo wa mawazo na kwamba, inaripotiwa kuwa takriban watu watano kati ya 10 wanaoishi na hali za kifafa wanapata maradhi ya wasiwasi au sonona na huwa katika hatari ya kufariki mapema mara tatu zaidi ya watu wa kawaida.

Alisema wengi wanaoishi na hali hizo wamekuwa hawaendi katika vituo vya afya kupata tiba sahihi, hivyo kuchangia usugu au ukali wa tatizo pamoja na madhara mengine.

"Tunaungana na serikali pamoja na taasisi zote za kijamii na za kitaaluma katika jitihada zao na kampeni za kuelimisha jamii kupata ufahamu sahihi kuhusu kifafa ili kutokomeza unyanyapaa," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Vitabu kufundishia, kujifunzia na mitaala mipya vyasambazwa

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imechapisha nakala 9,818,251 za muhtasari, vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu na kuvisambaza katika shule za msingi zinazotumia mtaala mpya kujifunza na kufundishia darasa la kwanza na la tatu.

Pia katika mwaka 2023/24, serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 ambao watapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu, ili kukidhi hitaji la ongezeko la wanafunzi nchini na kuboresha elimu .

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo jana bungeni jijini Dodoma, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacqueline Andrew, aliyehoji serikali ina mpango gani wa kuwezesha upatikanaji wa vitabu katika shule za msingi ambazo zimeanza mtaala mpya wa kingereza kuanzia darasa la kwanza.

Alisema katika nakala hizo, 509,582 ni za muhtasari na mtaala ulioboreshwa wa elimu ya awali, msingi na sekondari, 8,069,826 ni za vitabu vya kiada vya maandishi ya kawaida kwa darasa la awali, darasa la kwanza na la tatu kwa shule zinazotumia Kiswahili na Kiingereza kama lugha za kufundishia.

Prof. Mkenda pia alisema nakala 43,785 ni vitabu vya maandishi yaliyokuzwa 6,990 ni vitabu vya breli na nakala 1,183,568 za viongozi vya mwalimu vikiwa vimesambazwa kwa uwiano kati ya 1:2 hadi 1:4.

Akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Nora Mzeru aliyehoji ni lini serikali itaajiri walimu wa kutosha kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema inatarajia kuajiri walimu 12,000 kukidhi mahitaji hayo.

Alisema pia serikali imekuwa ikifanya jitihada kila mwaka kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari akitolea mfano kuwa katika mwaka 2020/21 hadi 2022/23, iliajiri walimu 29,879 wakiwemo 16,598 wa shule za msingi na 13,281 wa shule za sekondari.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janejelly Ntate, alihoji lini serikali itaajiri watalaam wa maabara katika shule za sekondari ili kuwapunguzia mzigo walimu wa sayansi kufanya kazi kama watalaam wa maabara.

Akijibu swali hilo, Mchengerwa alisema kati ya mwaka 2020/21 hadi 2022/23 serikali iliajiri wataalam wa maabara 165 ambao walisambazwa katika shule mbalimbali za serikali kadri ya mahitaji hata hivyo itaendelea kuajiri wataalam wa maabara kila mara nafasi za kuajiri zinapotolewa kulingana na upatikanaji wa fedha.

"Serikali inatambua umuhimu wa uwepo wa wataalam wa maabara shuleni. Wataalam wa maabara ni wasaidizi muhimu wa walimu wa masomo ya sayansi hasa katika kufundisha kwa vitendo," alisema

Aliwapongeza walimu ya sayansi nchini kwa kazi kubwa wanayoifanya kwani kwa sasa wamekuwa wakitumika kuandaa vifaa na kemikali kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo na mitihani kwa wanafunzi.


## TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD na ADILI AUCTION MART LIMITED** Kwa idhini na mamlaka waliyopewa na MWANGA HAKIKA BANK LIMITED, watauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo baada ya Siku saba (7), kumi na nne (14), siku ishirini na moja (21) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MARY AFANDE MWAIPOPO | MARY AFANDE MWAIPOPO | RESIDENTIAL LICENCE | MAKANGARAWE, MANISPAA YA TEMEKE | 23/05/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 2 | YOHANA MOSES MARIDAD | YOHANA MOSES MARIDAD | RESIDENTIAL LICENCE | BARABARA YA MWINYI,YOMBO VITUKA,MANISPAA YA TEMEKE | 24/05/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA MBILI ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 3 | SIMON YASINTO MILANZI | SIMON YASINTO MILANZI | RESIDENTIAL LICENCE | MBAGALA KUU,MWANAMTOTI,MANISPAA YA TEMEKE | 27/05/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 4 | VICENT SELINA MATONYA | VICENT SELINA MATONYA | RESIDENTIAL LICENCE | MWEMBE MADAFU ,UKONGA ,MANISPAA YA ILALA | 29/05/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA TATU ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 5 | ISIHAKA A SHAMASI | ISIHAKA A SHAMASI | RESIDENTIAL LICENCE | KIJICHI BUTIAMA | 31/05/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 6 | ESTHER MARCO MASHAURI | ESTHER MARCO MASHAURI | RESIDENTIL LICENCE | MAKANGARAWE YOMBO DOVYA,MANISPAA YA TEMEKE | 03/06/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA TATU ASUBUHI | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 8 | HUSNA RAMADHANI MAULID | DELVIS J WASEDA | SALES AGREEMENT | MGEULE JUU KATA YA BUYUNI,MANISPAA YA ILALA | 6/06/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 9 | ABUU IDDY RAMADHANI | IBRAHIM MUHARAMI MRISHO/MAUA ABDALLAH TAMAMBELE | SALES AGREEMENT | MTAA WA KILIMAHEWA JUU,KATA YA WAZO ,MANISPAA YA KINONDONI | 8/06/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 10 | RAYMOND SIMON BILUSHA | RAYMOND SIMON BILUSHA | SALES AGREEMENT | KILIMAHEWA JUU WAZO MANISPAA YA KINONDONI DAR ES SALAAM | 26/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | ADILI AUCTION MART LIMITED |
| 11 | MAUA H RAI | MAUA H RAI | SALES AGREEMENT | MTAA WA MJI MPYA KATA YA SARANGA MANISPAA YA UBUNGO DAR ES SALAAM | 20/06/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA | ADILI AUCTION MART LIMITED |
| 12 | HAFSA ABDALLAH MUSHI | HAFSA ABDALLAH MUSHI | SALES AGREEMENT | MBEZI LUIS MANISPAA YA KINONDONI DAR ES SALAAM | 20/06/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA | ADILI AUCTION MART LIMITED |
| 13 | MWAJUMA C MAGORI | ASIA ALLY GUBU | SALES AGREEMENT | NZASA A CHARAMBE MBAGALA MANISPAA YA TEMEKE DAR ES SALAAM | 28/06/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA | ADILI AUCTION MART LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada ata lazimika kulipa malipo yasiyo pungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hatimiliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa bank (eviction) niza mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTDP.O.Box 68172**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: 0620 848 565/ 0714 598 559**
**Email: lehalelglc@gmail.com**

**ADILI AUCTION MART LIMITED, S.L.P 40616, DAR ES SALAAM SIMU: 0675 056 267 / 0716 651 103**
**Email: info@adiliauction.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uelimishaji, uhamasishaji ni muhimu matumizi nishati safi

**JUKUMU** kubwa linalomkabili kila mwananchi hivi sasa ni umuhimu wa uelewa wa matumizi ya nishati safi katika jitihada za kupambana na uharibifu wa mazingira.

Katika hili kuna kila sababu ya kuongeza uelewa wa wananchi na taasisi kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kupitia programu mbalimbali za uelimishaji na uhamasishaji ili kuondoa fikra hasi zinazosababisha ukinzani kwa matumizi ya nishati hizo.

Ili kufanikiwa katika utekelezaji wa matumizi ya nishati hiyo ipo haja ya kufanyika kwa mijadala ya kitaifa, majukwaa yenye ushawishi, pamoja na elimu kuanzia ngazi ya chini ya kijamii.

Linapokuja suala la matumizi ya nishati safi ni lazima pia kuwapo na maandalizi ya kumwezesha mwananchi kuwa na vifaa vitakavyomwezesha kuvipata kwa gharama nafuu na kwa urahisi ili asiweze kushawishika kubaki kwenye matumizi ya kuni na mkaa ambayo ataona ni rahisi kwake na kuendelea kuharibu mazingira.

Vifaa hivyo ni pamoja na majiko sanifu ya kupikia kwa kupunguza tozo na kodi zinazotozwa katika nishati, kutoa ruzuku na kubuni mifumo ya kifedha na teknolojia ya kuwezesha watumiaji kumudu gharama za nishati hiyo kwa kuzingatia kipato chao.

Vilevile, kuoanisha na kuhuisha sera, sheria, kanuni na miongozo wezeshi itakayofanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kuandaa miongozo ya viwango vya ubora wa nishati, vifaa na majiko ya kupikia, kuweka mifumo na kanuni za usimamizi wa mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia, pamoja na kujumuisha masuala ya nishati safi ya kupikia katika mipango ya matumizi ya ardhi na ujenzi wa majengo ya makazi na biashara.

Kuhamasisha uwekezaji katika nishati safi ya kupikia kwa kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kutumia fursa za biashara zilizopo katika mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia, na kuhamasisha matumizi ya mifuko ya fedha na programu za kitaifa katika kukuza na kuendeleza uwekezaji nchini.

Jitihada hizi zinajumuisha uandaaji wa kanzidata ya takwimu na taarifa kuhusu nishati safi ya kupikia, mikopo yenye riba nafuu na kuhamasisha biashara ya kaboni katika miradi ya nishati safi ya kupikia.

Katika kuhakikisha kuwa jambo hili linafanikiwa ni muhimu kuwajengea uwezo watekelezaji wa miradi ya nishati safi ya kupikia kwa kutoa elimu ya ufundi na mafunzo stadi kuhusu nishati hiyo na kutoa elimu na kufunga miundombinu ya kupima viwango vya ubora wa nishati, vifaa na majiko ya nishati safi ya kupikia, mafunzo kwa wajasiriamali kuhusu matumizi yake na kuzingatia ushiriki wa wazawa katika miradi yake.

Vilevile, kujumuisha masuala ya nishati safi katika mitaala ya kufundishia shuleni ili kujenga kizazi chenye uelewa. Aidha, utendaji kazi wa idara ya usimamizi wa biashara ya kaboni uimarishwe kupitia mafunzo ili kuongeza wigo wa utafiti na ubunifu wa teknolojia zinazohusu nishati ya kupikia kwa kuimarisha ushirikiano kati ya wawekezaji wa nishati safi ya kupikia na taasisi za utafiti na maendeleo pamoja na kutoa mafunzo kwa wakufunzi.

Pia, kutenga bajeti katika uendelezaji wa utafiti, ubunifu na uvumbuzi wa teknolojia zinazohusu nishati safi ya kupikia, kujumuisha masuala ya usawa wa kijinsia kwa kuhamasisha ushiriki wa wanawake na vijana katika mnyororo wa thamani wa nishati hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Madiwani, pia kaka na dada zenu wabunge, igeni hili nililoliona Bonyokwa ya Dar

Na Halfani Chusi

**KUNA** jambo fulani hata rais mwenyewe aliomba, akiwataka viongozi walioko katika nafasi zao, wafike waliko wananchi kusikia kero zao na kuzifanyia kazi 'akiwapiga' na msamiati 'msijifungie ofisini.' Hiyo nilipenda!

Nikirejea huku ninakoishi katika Kata ya Bonyokwa majirani zake ni waambiwe wamuige Diwani wa Kata ya Bonyokwa, Tumike Malilo aliyeamua kuiga mfumo wa viongozi wake wa juu kuitisha mkutano wa hadhara na kusikiliza kero za wanakata wake.

Ilizoeleka kuwaona viongozi wakubwa ndio wakifanya ziara, lakini safari hii nimemshuhudia diwani huyo akifanya hivyo, walimpigia kura wakiwa katika bashasha kufurahia tukio hilo.

Kilichonivutia zaidi, ni kuona wananchi wameitikia wito na kuanza kuwailisha vilio vyao na wengine walijibiwa papohapo na kutafutiwa ufumbuzi.

Aliyefungua pazia la kuwasilisha kero Jacob Jailosi, alisema kero kubwa inayowakabili wana - kata hao ni ubovu wa miundombinu ya Barabara, huku akisisitiza ni jambo linalokwamisha shughuli za uchumi kwa kiasi kikubwa.

"Barabara ni mbovu, kutoka hapa kwenda kimara unatumia muda mwingi ikinyesha mvua ndio balaa hakupitiki kabisa, vivuko kwa maana ya madaraja vimejengwa kwa kiwango cha chini.

"Madaraja mengi hayavuki na hatujaambiwa lini tatizo hilo litakwisha tunaiomba Serikali itusaidie katika hili," akasema

Mwingine aliyepokea kijiti cha kuwasilisha kero, Jane Juma, anasema katika kata hiyo kuna changamoto ya kukatika maji kila mara mara, akisistiza ni jambo linalowatesa kinamama.

"Maji yanakatika kila siku na wakati nmwingine yanatoka kidogo Rais Samia Suluhu Hassan alisema lengo lake ni kumtua mama ndoo kichwani lakini hatuoni tunaomba serikali itusaidie kutatua kero hii," analalamika

Kilichowakuna wana-kata zaidi, ni namna diwani wao alivyoanza kujibu hoja zao, akianza kwa ufafanuzi wa fedha za mradi wa kujenga Barabara kutoka Kinyerezi kupitia Bonyokwa mpaka Kimara, pia barabara kutoka Segera Magereza mpaka Bonyokwa, ambayo nayo ujenzi umeanza na imeshawekwa katika kipande kimojawapo.

Pia, Barabara ya kutoka Masia mpaka Baampya, ikiwa kwenye mpango wa kujengwa mwaka huu na kawamba kinachosubiriwa ni kupungua kwa mvua zinazoendelea kunyesha.

Kuhusu kero ya maji, akaeleza: "Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), wamesema pampu iliyopo ni ndogo kuweza kusukuma maji ili yawafikie wananchi wote kwa wakati lakini wameshaagiza nyingine mpaka mwisho wa mwezi itakuwa imefika kwa hiyo, tarajieni kupata maji safi."

Katika mkutano huo, hakumwacha nyuma Ofisa Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Sam Swila, naye alimuunga mkono kushirikiana na wana-Bonyokwa kutatua kero zilizo wasilishwa na baadhi ya wananchi katika mkutano huo.

"Katika mkutano huu, wapo watu wa DAWASA kwa ajili ya kuelezea kero ya maji pia watu wa TARURA kwaajili ya ubovu wa miundombinu kwahiyo nitasimamia kikamilifu kuhakikisha ahadi na malengo yaliopangwa yanatimia kwa wakati. amesema Mtendaji huyo ambaye alishinda tuzo ya mfanyakazi bora katika siku ya sherehe ya Mei Mosi.

Diwani huyo alimwinua mkutanoni, Mhandisi wa TARURA Wilaya Ilala, Fadhili Sadala, kutaja mikakati iliyopo kwa wananchi kuhusu ujenzi wa barabara katika kata hiyo naye akajibu: "Ipo bajeti imetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara zinazopita maeneo haya tunasubiri mvua ipungue tuanze ujenzi" alijibu

Ni aina ya mkutano uliokuwa na mengi wananchi wakipata nafasi ya kuchangia hoja bila bughudha na hata kutoa ushauri wa namna ya kuibadilisha Bonyokwa.

Ni vyema mfunmo huu ukaigwa na madiwani wote na sio kusubiri mpaka Mbunge au kiongozi wa juu afike itasaidia kutatua matatizo ya wananchi kwa haraka zaidi na kuliletea Taifa maendeleo.

## HABARI KITAIFA



Wakazi wa Mtaa wa Upendo, Kata ya Saranga, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam, wakipita katika daraja la Moa jana, ambalo limeanza kutitia kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, kitendo kinachohatarisha usalama wa watumiaji wa daraja hilo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Waliotafuna mamilioni wakalia kuti kavu

**Na Munir Shemweta,** MLELE

MKUU wa Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, Alhaj Majid Mwanga, amesema wahusika wote wa ubadhirifu wa Sh. 39,501,665 katika kijiji cha Kibaoni, Halmashauri ya Mpimbwe Wilaya ya Mlele, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Alhaji Mwanga asema hayo juzi katika mkutano wa hadhara na wananchi wa kijiji cha Kibaoni wakati wa uwasilishaji taarifa ya uchunguzi wa mapato na matumizi iliyotokana na migogoro ya ardhi katika kijiji hicho iliyosomwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mpimbwe, Shamim Daud.

"Hatutamfumbia macho mtu hata tone moja. Baadhi ya viongozi wa kijiji nao wamehusika kwenye upotevu wa Sh. 39, 501, 665. Wote hao walihusika lakini na watu ambao ni nje ya serikali ya kijiji walihusika kama ilivyosemwa mmoja wa watumishi yuko kampuni hiyo," alisema.

Akiwasilisha taarifa ya uchunguzi wa mapato na matumizi iliyotokana na migogoro ya ardhi kwenye kijiji hicho, Daud alisema maeneo yaliyohusika katika ubadhirifu ni pamoja na eneo la shule mpya ya Kibaoni ambapo wakati wa kupatikana kwake zilipunguzwa ekari tatu kutoka 18 na kuwa 15.

Eneo lingine, kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, ni la viwanda vidogo (SIDO) ambalo Sh. milioni 8.8 kwa ajili ya mauzo ya viwanja 48 hazikupelekwa benki na hakuna matumizi yoyote yaliyoonekana ya shughuli za serikali.

Pia alisema makusanyo ya mapato ya Sh. 21,240,000 kutoka vyanzo vya mapato mbalimbali ya kijiji cha Kibaoni, yanayojumuisha michango ya jamii, kukodisha mashamba, tozo na faini mbalimbali, ni Sh. milioni mbili tu zilizopelekwa benki wakati Sh. 19,210,000 hazikupelekwa.

"Kumetokea pia ubadhirifu wa fedha za kijiji kutoka katika akaunti yake ya jumla ya milioni 2.80 zilizotolewa katika kaunti kwa ajili ya kurejesha kwa watu 39 wakati hakuna fedha yoyote iliyoingizwa kutokana na tukio hilo". Alisema Shamim.

Kuhusu malipo ya fidia kwa serikali ya Kibaoni kutokana na maeneo ya wananchi kuchukuliwa na kuchimba vifusi na kuchukua udongo kwa ajili ya ujenzi wa barabra ya Kibaoni- Sitalike, alisema Sh. milioni 21 zilipokewa kutoka kampuni ya RSG Ltd na wananchi wawili nao kufidiwa lakini pesa zote hazikupelekwa benki.

Kwa mujibu wa ripoti ya uchunguzi, baadhi ya viongozi wa kata, watendaji wa vijiji na watumishi wa kampuni ya RSG walishiriki kugawana fedha za fidia.

Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Kibaoni, wlitaka hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika kwenye ubadhilifu wa fedha hizo pamoja na kuzirejesha.

"Hizi pesa zote zirudi ili kupunguza msongamano wa mizigo iwe kuuzwa nyumba, iwe kiwanja au kufanya nini ili anayekuja leo Kibaoni ajue anapoondoka hata Sh. 500 ya wizi ajue inaweza kumuunguza," alisema Mathelius Matabula, mkazi wa Kibaoni.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ni Mbunge wa Kavuu, Geophrey Pinda, alitaka sheria ifuate mkondo wake huku akisisitiza fedha zilizoibwa zirudi kwa wananchi kwa kuwa tangu fedha hizo zipotee miradi mingi imesimama.

Kutokana na ripoti hiyo, Alhaj Mwanga amemwelekeza mkurugenzi kuchukua hatua kwa watumishi wote waliohusika sambamba na kuiarifu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Jeshi la Polisi kuwakamata wote waliohusika na kuchukua hatua.

Novemba 3, 2023 Mkurugenzi wa Halmashauri alielekeza ufanyike ukaguzi wa mapato na matumizi ya kijiji cha Kibaoni ikiwa ni pamoja na kuhakiki hoja zilizoibuliwa kwenye taarifa ya kamati huru ya uchunguzi wa migogoro ya ardhi ya kijiji.

Kazi ya ukaguzi ilianza Novemba 9, 2023 na kukamilika Machi 25, mwaka huu na miongoni mwa mambo yaliyobainika ni kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha za umma na matumizi mabaya ya madaraka yaliyosababisha baadhi ya viongozi wa kata, viongozi na wajumbe wa serikali ya kijiji pamoja na watumishi kujinufaisha kwa kujigawia viwanja bila kufuata taratibu.

# Polisi yasaka watu walioua mwanafunzi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamsaka mtu/watu waliohusika na mauaji ya mwanafunzi Angela Mseven (8) wa darasa la pili Shule ya Msingi Carisa iliyopo Mwendapole Wilaya ya Kibaha.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka eneo hilo, mwanafunzi huyo alikuwa anacheza na watoto wenzake eneo hilo na baadaye kukutwa amefariki kwenye shimo hilo.

Kamanda wa polisi mkoa wa Pwani, Kamishna msaidizi Mwandamizi (SACP) Pius Lutumo, aliwaambia waandishi juzi kuwa jeshi hilo lilipokea taarifa kuhusiana na mtoto huyo kuzama maji katika shimo la maji taka na kufariki dunia.

Alisema uchunguzi wa awali wa jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya kiuchunguzi na kubaini kuwa mtoto huyo aliuawa na kisha kutumbukizwa katika shimo hilo tofauti na taarifa iliyowasilishwa awali.

Kamanda Lutumo alisema kutokana na uchunguzi huo, jeshi limeanza kuwatafuta waliohusiaka na tukio hilo huku likitoa taarifa kwa wananchi wenye taarifa sahihi kuhusiana na tukio hilo kujitokeza kutoa ushirikiano kuwakamata watuhumiwa.

Mei 7, mwaka huu, ilisambaa taarifa kwenye mitandao ya jamii ikieleza kupotea kwa mwanafunzi huyo aliyeondoka nyumbani akienda kucheza na wenzake.

Hata hivyo muda mfupi ilisambaa taarifa nyingine ikithibitisha kupatikana mwili wa mtoto huyo kwenye shimo la maji karibu na nyumbani kwao.

**Mei 7, mwaka huu, ilisambaa taarifa kwenye mitandao ya jamii ikieleza kupotea kwa mwanafunzi huyo aliyeondoka nyumbani akienda kucheza na wenzake.**

twiga cement
Heidelberg Materials

**TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY**
**TAARIFA KWA WANAHISA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa wote wa Tanzania Portland Cement Public Limited Company kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa utafanyika:

**Johari Rotana Hotel, Ukumbi wa Almasi, Ghorofa la Sita**
**Sokoine Drive, Dar es Salaam,**
**siku ya Jumatano, tarehe 5 Juni 2024, saa nne asubuhi.**

**DONDOO**

1. Ufunguzi wa Mkutano: Katibu kusoma taarifa iliyotolewa kuuita Mkutano Mkuu na kuhakiki kama akidi ya Mkutano imetimia.
2. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 31 uliofanyika tarehe 31 Mei 2023.
3. Kupokea, kujadili na kama zitaafikiwa kupitisha taarifa ya wakurugenzi, taarifa ya wakaguzi na taarifa ya fedha kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2023.
4. Kupokea, kujadili na kama litaafikiwa kuthibitisha gawio la mwaka 2023.
5. Kuthibitisha uteuzi wa wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka unaoisha tarehe 31 Desemba 2024.
6. Kujadili mambo mengine ya kampuni ambayo taarifa zake zimepokelewa.

**Kwa Niaba ya Bodi**
**Tarehe: 10 Mei, 2024**

**Katibu wa Kampuni**
1. Mwanahisa yeyote aliye na haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, anaruhusiwa kuteua mwakilishi au wawakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Fomu ya kuteua mwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya kampuni **(https://www.twigacement.com).**
2. Mwakilishi atakayeteuliwa siyo lazima awe mwanahisa wa kampuni. Fomu ya kuteua mwakilishi ambayo imejazwa na mwanahisa inatakiwa iwasilishwe kwenye ofisi za kampuni, Wazo Hill, Dar es Salaam angalau masaa 24 kabla ya muda wa kuanza mkutano, la sivyo fomu itakuwa haijakidhi vigezo.
3. Kwa ajili ya utambulisho, mwanahisa anatakiwa kuja na cheti cha umiliki wa hisa pamoja na kitambulisho chake (pasi ya kusafiria, leseni ya udereva, au kitambulisho cha taifa, cha kazi, au cha mpiga kura).
4. Mahesabu kamili ya kampuni, ambayo yamepitishwa na wakaguzi, yanapatikana kwenye ofisi za kampuni, Wazo Hill, Dar es Salaam, au pia kupitia tovuti ya kampuni **(https://www.twigacement.com).**

# Adaiwa kumbaka mwanafunzi wake

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Katoro (jina linahifadhiwa) miaka36 anadaiwa kumbaka mwanafunzi wa kidato cha tatu alipomtuma nyumbani kwake kisha kumfuata na kumfanyia ukatili huo.

Tukio hilo limethibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Safia Jongo, huku akibainisha kuwa lilitokea Mei 2, mwaka huu.

Kamanda Jongo alisema siku ya tukio, mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa), alikuwa darasani ndipo mwalimu huto alimwagiza kwenda nyumbani kwake kumchukulia kitu huku akimfuata kwa nyuma.

Alisema binti huyo alipofika nyumbani kwa mwalimu huyo, alishtuka kuona mlango unafungwa kisha kuanza kufanyiwa ukatili na mwalimu huyo.

SACP Jongo alisema baada ya tukio hilo, mwanafunzi alikwenda kutoa taarifa kwa mkuu wa shule kwamba mkuu huyo kwa kushirikiana na mtuhumiwa, walimtisha kuwa watamwadhibu kama atatoa taarifa sehemu yoyote.

"Tulipata tarifa Mei 5 na kuchukua hatua ya kumkatamata mtuhumiwa pamoja na mkuu wa shule na baada ya hapo, utaratibu wa kisheria unaendelea na hatua zaidi zitachukuliwa dhii yao baada ya kukamilisha uchunguzi," alisema Kamanda Jongo.

Aidha, kamanda huyo aliwataka wazazi, walimu na walezi kuwa na tabia ya kuwahoji watoto wanapotoka shuleni ili kama kuna matatizo wanakumbana nayo, wayabaini mapema.

Katika hatua nyingine, Kamanda Jongo alithibitisha kutokea kwa tukio la mtoto Kazungu Julius (10) mwenye ualibino na mwanafunzi wa Shule ya Msingi Katoro, kujeruhiwa kwa kukatwa na mapanga maeneo mbalimbali ya mwili ikiwemo kichwani na mikononi na mtu aliyekuwa amefunika uso wake.

SACP Jongo alisema tukio hilo lilitokea Mei 4, mwaka huu saa 2:00 usiku, wakati mtoto huyo alipotoka nje baada ya kutumwa na mama yake, ndipo alipovamiwa na mtu huyo aliyeanza kumjeruhi kisha kutokomea kusikojulikana.

Alisema kwa mujibu wa uchunguzi wa awali, tukio hilo ni la kupangwa na wala si la imani za kishirikina za kuhitaji kuondoka na kiungo chochote cha kijana hiyo.

"Mtu huyu tunaendelea kumsaka popote atakapokuwa. Lakini pia niwatoe hofu wananchi na watu wenye ualibino kuwa na amani kwani kwa mujibu wa daktari, mtu huyo hakuwa na nia ya kuondoka na kiungo chochote kutokana na majereha pamoja na aina ya panga lililokutwa eneo la tukio," alisema Kamanda Jongo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Prof. William Palangyo (kulia), akitiliana saini makubaliano ya ushirikiano na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa (kushoto), jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa chuo hicho. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yakemea wanaotoza ushuru wateja wadogo wa samaki

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imekemea vikali tabia ya baadhi ya wasimamizi wa mialo ya samaki kuwatoza ushuru wateja wanaonunua chini ya kilo 30 kwa matumizi ya nyumbani na kuziagiza halmashauri kukomesha jambo hilo kwa kuwa ni kinyume cha sheria.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, aliyasema hayo juzi wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira, aliyehoji serikali ina mikakati gani wa kupunguza na kufuta baadhi tozo ili kuleta unafuu kwa wal-imu.

Alisema sheria inaelekeza wafanyabiashara wa samaki kutozwa ushuru hata wakinunua chini ya kilo 30, lakini wateja wa kawaida wanaonunua kwa matumizi ya nyumbani hawapaswi kutozwa isipokuwa wakinunua zaidi ya hapo.

Mnyeti alisema mwaka 2020 na 2022 serikali ilifanya maboresho ya tozo mbalimbali, ikiwamo baadhi ya leseni kuunganishwa na tozo zingine kupunguzwa na wizara itaendelea kuboresha na kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi kadiri itakavyowezekana na kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi nchini.

"Tozo ambazo zilipunguzwa ni ushuru wa dagaa wanaozalishwa Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi kutoka Dola 0.16 (Sh. 412.6) hadi Dola 0.1 (Sh.257.9) kwa kilo na tozo ya dagaa wa Ziwa Tanganyika kutoka Dola 0.5 (Sh. 1,289.33) hadi Dola 0.3 (773.6) kwa kilo," alisema.

Alitaja tozo zingine zilizobadilishwa kuwa ni za kusafirisha minofu ya sangara nje ya nchi iliyopunguzwa kutoka Dola 0.2 (Sh. 515.7) hadi Dola 0.1 (Sh. 257.9) kwa kilo.

Pia alisema serikali imepunguza ushuru wa uingizaji mazao ya bahari kutoka Dola 2.5 (Sh.6,446.6) hadi Dola 0.5 (Sh.1289) kwa kilo kwa ngisi, pweza na kaa na gharama ya ada za leseni za kusafirisha dagaa kutoka Dola 1,000 (Sh. 2,578,650) hadi Dola 250 (Sh. 644,663) kwa dagaa wa maji chumvi na maji baridi.

## BRELA, taasisi tatu kulinda miliki bunifu

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetia saini makubaliano na taasisi tatu kwa ajili ya kukuza na kulinda kazi za ubunifu.

Taasisi hizo ni Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) na Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana mbele ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma, kwenye maadhimisho ya kimataifa ya Siku ya Miliki Bunifu.

Akizungumza baada ya hafla hiyo, Mkuu wa TIA, Prof. William Pallangyo, alisema makubaliano hayo yatakuwa na manufaa makubwa kwenye maendeleo ya taasisi hiyo.

Alisema wanaamini kupitia ushirikiano huo, wataongeza nguvu katika kazi za utafiti zinazofanywa na taasisi pamoja na kazi za ushauri na msaada wa kiufundi.

Prof. Pallangyo alisema BRELA itawasaidia wanafunzi kupitia hatua mbalimbali za kusajili ubunifu wanaofanya kwa kuwa wengi kwa sasa hawajui cha kufanya ili kulinda na kuendeleza kazi zao kisheria.

"Wanafunzi wetu watanufaika sana na ushirikiano huu kwa sababu wanapokuwa na ubunifu wanashindwa kulinda kwa sababu hawana elimu ya nini cha kufanya," alisema.

Alisema kupitia ushirikiano huo, wataandaa na kushiriki semina na makongamano mbalimbali ambayo yatasiadia kwa kiwango kikubwa kukuza uelewa wa wanafunzi na walimu kuhusu mambo yanayohusu hatimiliki, usajili na uendeshaji wa biashara kitaaluma na kulinda ubunifu wa vijana wabunifu na wagunduzi.





## Maelfu wafurika ofisi ya Makonda wakidai haki

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

WANANCHI zaidi ya 1,500 wamefurika katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, kwa ajili ya kutaka kupatiwa haki zao ambazo wanazitafuta kwa muda mrefu bila mafanikio.

Wananchi hao walianza kuingia katika ofisi hiyo kuanzia majira ya saa 10 alfajiri huku wengine wakiwa na nyaraka walizozishikilia mkononi na kisha kupatiwa namba kwa ajili ya kukaa foleni.

Makundi tofauti yalijitokeza ikiwemo wanawake, wazee, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya kutii agizo la Makonda la kuwataka wajitokeze kupata haki zao.

Baadhi ya wananchi wanaoishi katika maeneo ya mbali waliamua kulala mjini ili kuwahi foleni na wengine wametokea mikoa ya jirani kutaka kueleza changamoto zao wakiamini zitatatuliwa katika kliniki hiyo waliyotangaziwa ya siku tatu mkoani Arusha.

Mabanda mbalimbali ya taasisi yalikuwa yamewekwa nje ya ofisi hiyo kwa ajili ya kuanza kusikiliza wananchi ambao ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Arusha, dawati la jinsia, Shirika la Umeme (Tanesco), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), timu ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Arusha, polisi, wadau wa kutoa elimu kisheria na kampuni za kisheria 70.

Wananchi hao walianza kuitwa kwa namba na kuelekea katika banda ambalo unashida nalo ili changamoto yao itatuliwe. Akizungumza na waandishi wa habari, Makonda alisema kwenye kusimamia haki za wananchi yupo tayari kupoteza chochote ilimradi mtu mmoja apate haki yake.

"Kwenye haki ya mtu cheo hakina thamani, kwenye haki ya mtu umaarufu wangu hauna thamani, kwenye haki ya mtu heshima niliyonayo haina thamani maadamu Mungu amenipa uhai akaniruhusu kuwapo hapa nitasimama na mwananchi niwaombe watendaji mtende haki," alisema Makonda.

Aidha, aliagiza endapo kuna mtendaji aliyehusika kwenye kesi ya mwananchi ambaye hajafika katika eneo la tukio atafutwe haraka na kufika.

Makonda alisema hata kama kuna mtu una kesi ipo mahakamani na haelewi mwenendo wa kesi unavyokwenda inawezekana ni maskini, mama mjane, mtoto yatima ama mzee wote watasaidiwa kupata wanasheria.

# Wawili jela miaka 20 kwa kukutwa na nyama ya twiga

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara imewahukumu watu wawili kwenda jela miaka 20 kila mmoja kwa kosa la uhujumu uchumi.

Wawili hao walikuwa wakituhumiwa kwa kukutwa na kichwa cha twiga, ngozi, pamoja na kilo 40 za mnyama huyo.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Victor Kimario, baada ya kusikiliza pande zote mbili.

Aliwataja washtakiwa kuwa ni Paulo John (23) mkazi wa Kijiji cha Mapea na Athuman Misanya(31) mkazi wa Mamire.

Kimario alisema washtakiwa hao walitenda kosa hilo Februari 2, mwaka huu katika eneo la Hifadhi ya Burunge, ikiwa ni kinyume na Kifungu cha 86(2) (C) cha Sheria ya Wanyamapori, Sura 283 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022 ikisomwa pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi Kifungu cha 60(2) Sura 200 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Alisema washtakiwa wote walikuwa na vidhibiti hivyo wakiwa wamebeba kwenye ndoo.

Kimario alisema shahidi namba moja na namba mbili waliithibitishia Mahakama kuwa walikuwa wanne ila wengine walitoroka.

"Wote walikiri walikutwa porini kuchukua samaki japo wao wanadai ni samaki ila ilikuwa ni nyama ya twiga, hapana shaka kuwa ilikuwa nyama ya twiga," alisema Kimario.

Alisema upande wa mashtaka umethibitisha pasipo na shaka kuwa washtakiwa walikutwa na nyara za serikali licha ya wao kusema ni samaki.

Wakili wa serikali kutoka Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA), Getrude Kariongi, alisema hawana kumbukumbu za nyuma za watuhumiwa hao kufanya makosa ila kitendo cha kuua twiga ni kuharibu nembo ya Taifa.


Alisema kumtoa mnyama kwenye ikolojia ni kuathiri wanyama wengine wakati twiga ni kivutio cha watalii na aniingizia Taifa mapato.

Vile vile alisema nyama waliyokamatwa nayo ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani 20,000 (Sh.milioni 50).

Hivyo, aliiomba Mahakama hiyo kuitaifisha pikipiki waliyokutwa nayo na ndoo ili ziwe mali ya serikali.

Wakili wa utetezi, Festo Jackson alisema ni wateja wake ni mara ya kwanza wanatenda kosa kama hilo, umri wao ni nguvu kazi ya Taifa na wana wategemezi, hivyo aliiomba Mahakama hiyo kuwapunguzia adhabu.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Hakimu Kimario alisema nguvu walizokuwa nazo washtakiwa walizitumia vibaya kuihujumu serikali kwa kuua twiga ambaye ni nembo ya Taifa.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainab Abdallah (wa pili kushoto), akipata maelezo kuhusu mfumo wa ulipaji kodi kutoka kwa maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), alipofanya ziara ya kuwatembelea wafanyabiashara akiongozana na maofisa wa mamlaka hiyo, wilayani humo juzi. Kulia ni Meneja wa TRA wa wilaya hiyo, Daud Njohole na (wa pili kulia) ni Meneja wa TRA Mkoa wa Tanga, Thomas Masese. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Ukuaji utalii kwawavutia wanasayansi, w'biashara kimataifa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KASI ya ukuaji wa sekta ya utalii nchini imeanza kuwavutia wanasayansi na wafanyabiashara wa kimataifa kulipigia chapuo, Shirika la Hifadhi za Taifa 'TANAPA, Jumuiya ya Waongozaji wa Utalii na Mawakala wa Utalii kutoyakwepa maendeleo ya kidijitali.

Badala yake wameshauri ili kuepusha matukio ya ujangili wa wanyamapori, watalii kupoteana na waongoza utalii na kuwasaidia mawakala wa utalii kujua wageni wamefika kituo gani na kama wako salama, hawawezi kuepuka matumizi ya teknolojia ya QR Codes Track (misimbo milia) kama zinavyofanya nchi nyingine duniani.

Jana, mwanasayansi kutoka Singapore, Rangesh Nallan, ambaye ni mmiliki wa kampuni ya Digiticket Afrika, alisema rekodi ya Tanzania kupokea watalii milioni 1.8, sawa na asilimia 118 kwa mwaka jana, ikiwa ni ongezeko la asilimia 32 kabla ya ugonjwa wa UVIKO-19, inapaswa kwenda sambamba na uwekezaji wa maendeleo ya dijitali ya misimbo milia ili kuvutia watalii wengi duniani.

"Tanzania sasa inapaswa kuiga mataifa mengine yanayoendesha sekta ya utalii kwa mafanikio kama Afrika ya Kusini, ambayo inatumia huduma ya misimbo milia kwa watalii wanaoingia kwao," alisema.

Akizungumzia teknolojia hiyo, mwongozaji wa utalii, Hollyfield Mbona, alisema ujio wa teknolojia hiyo ya misimbo milia, ni moja ya utatuzi wa changamoto kubwa ya Tanzania, kukabiliana na ongezeko la kasi ya watalii, baada ya Filamu ya 'The Royal Tour' iliyotengenezwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Mkurugenzi wa SkyNet Solutions, Epifan Benard, alisema wameingia makubaliano ya kufanya kazi na kampuni ya QR Codes 4you ya nchini Singapore, ambayo inataka kutoa huduma hiyo ya misimbo milia kwenye sekta ya utalii nchini.

Kwa mujibu wa Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, mwaka 2023, watalii waliongezeka kutoka nchi za Marekani kwa asilimia 16, Italia asilimia 8, Canada 7.6, Uingereza 5.9 na Ufaransa 5.4.

Wakati watalii kutoka nchi za Afrika, waliongezeka kutoka nchi za Zambia, Kenya, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Aidha, alisema mapato ya nchi kupitia sekta ya utalii, yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 3.5 hadi Dola za Marekani 3.4 ikiwa na ongezeko la Dola za Marekani bilioni 1.5

Kairuki, alisema serikali inaendelea na juhudi za kutangaza zaidi utalii ili kupata watalii wengi kutoka katika nchi za China, India, Urabuni na Amerika ya Kusini.



# Wanahabari watwishwa zigo utunzaji mazingira

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAANDISHI wa habari mkoani Mwanza wamekumbushwa kuibeba na kutekeleza kwa vitendo ajenda ya utunzaji wa mazingira, kuufahamisha umma juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi na namna ya kukabiliana nazo.

Rai hiyo imetolewa juzi na wanataaluma wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya habari Duniani, yaliyofanyika kimkoa katika Chuo Kikuu cha Mt. Agustino Tanzania (SAUT).

Mhadhiri kutoka Kitivo cha Mawasiliano, Idara ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma SAUT, Tabu Manyama alisema vitu vitatu vinavyosababisha ongezeko la umasikini duniani ni pamoja na uharibifu wa mazingira.

Alitaja vitu vingine kuwa vita na milipuko ya magonjwa hatari ambavyo hata hivyo aliviweka katika dhana moja ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hivyo alisema kufuatilia hali hiyo ni jukumu kwa vyombo vya habari kuweka jicho la karibu katika kuelimisha jamii juu ya namna ya kukabiliana na hali hiyo.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa Mwanza, Edwin Soko alisema tatizo la uharibifu wa mazingira limesababisha mabadiliko ya tabianchi na athari zake tayari zimeanza kuonekana.

Alitaja athari hizo kuwa ni pamoja na mafuriko katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi ambayo yamekuwa janga la dunia kwa sasa.

Alisema kaulimbiu ya maadhimisho hayo mwaka huu ambayo ni uandishi wa habari na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, imelenga kutoa msukumo kwa waandishi wa habari kubeba wajibu wa kuelimisha jamii kuhusu utunzaji mazingira.

Makamu Mkuu wa SAUT, Prof. Costa Ricky Mahalu, aliwataka waandishi wa habari kutumia weledi katika kuleta mabadiliko katika jamii hususani katika masuala ya utunzaji mazingira kwani jamii ina imani kubwa na kazi inayofanywa na waandishi wa habari.

Mwanafunzi wa masomo ya uandishi wa habari kutoka SAUT, Fidelis Seleman alisema uandishi wa habari za mazingira unasaidia jamii kupata elimu na hatua salama za kuchukua wakati wa majanga kama mafuriko au kimbuka na kutoa rai kwa wananchi kutambua umuhimu wa habari hizo.

Mei 3, mwaka huu Tanzania iliungana na mataifa mbalimbali duniani kuadhimisha siku hiyo ambayo kitaifa yalifanyika jijini Dodoma yakiongozwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.




Wafanyabiashara wadogo maarufu Machinga wakifanya shughuli zao katika eneo la Kimara Mwisho, Dar es Salaam jana, licha ya kuwapo bango lenye ujumbe unaowazuia kufanya hivyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wachimbaji madini walia athari zebaki

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WACHIMBAJI wa dhahabu katika mgodi wa Mwakitolyo uliopo Kata ya Mwakitolyo wilayani Shinyanga, wameeleza athari ya matumizi ya kemikali ya zebaki wakati wakichenjua ikiwa ni pamoja na kupata ulemavu wa ngozi.

Walibainisha hayo juzi wakati wa mafunzo ya matumizi salama ya kemikali ya zebaki kwa wachimbaji wadogo na wasambazaji, iliyokuwa yanatolewa na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Ofisi ya Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mmoja wa wachimbaji hao, Juma Daudi alisema ukosefu wa elimu juu ya matumizi salama ya kemikali ya zebaki inasababisha wengi wao kupata madhara ambayo hayana tiba kutokana na kufanya shughuli hizo bila kuchukua tahadhari yoyote.

Mchimbaji mwingine Charles Misalaba alisema yeye ni miongoni mwa waathirika wa kemikali ya zebaki, kwamba amekuwa mtu wa kupoteza kumbukumbu kuwa na hasira muda wote na kuwa na msongo wa mawazo.

Hivyo aliiomba serikali kuangalia namna ya kumsaidia kupata tiba yake ili kuondokana na adha hiyo.

Meneja wa Ukaguzi na Usajili kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Dodoma, Magdalena Mtenga, alisema kunakiwango cha zebaki kinachoruhusiwa kuwa mwilini ila kinapozidi unatakiwa kuacha shughuli za uchenjuaji na kufanyakazi nyingine kwani tatizo hilo halina dawa.

Hata hivyo alibainisha kuwa baadhi ya madhara yanayowapata wachimbaji pindi wasipochukua tahadhari kuwa ni pamoja na kuathirika kwa mfumo wa fahamu, figo, uwezo wa kuona, mikono kutetemeka, mimba kutoka, watoto kuzaliwa na utindio wa ubongo na kuchanganyikiwa.

Awali Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa mradi huo kutoka NEMC, Hassan Maalim alisema wanatekeleza mradi wa kudhibiti matumizi ya zebaki kwa wachimbaji ili waweze kuwa na mazingira yenye viwango vinavyohitajika kwa mujibu wa mkataba wa Minamata.

Alisema mradi huo wanautekeleza katika mikoa ya Geita, Mbeya, Singida, Mwanza, Mara, Songwe na Shinyanga kwa sababu wengi wao wanafanya kazi katika mazingira magumu bila kuchukua tahadhari yoyote.

# DC ageuka ‘mbogo’ mrundikano wa taka sokoni

**Na Alex Sayi,** MASWA

MKUU wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, ameitaka Ofisi ya Usafi wa Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu kuacha ubabaishaji katika usimamizi wa shughuli za uzoaji taka.

Amesema ubabaishaji huo unasababisha kukithiri kwa uchafu wilayani Maswa.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi pamoja na wafanyabiashara wa Soko Kuu Maswa wilayani hapa alipotembelea kuona hali ya uchafuzi wa taka.

Pamoja na mambo mengine aliuagiza uongozi wa Halmashauri ya Maswa kujitathmini juu ya utendaji kazi wao kwa kuwa maelekezo yake ya kusimamia suala la usafi yamekuwa hayafanyiwi kazi na watendaji hao.

“Natoa saa mbili taka hizi ziondolewe hapa, suala la kusema trekta halina mafuta mara bovu sitaki kusikia, hivi wananchi wanatuelewaje? tunaposema trekta halina mafuta haya magari ya Halmashauri yamefikaje hapa? haya yanatoa wapi mafuta? au mnaona raha sisi kutukanwa na wananchi?,” alihoji Kaminyoge.

Aidha, aliwataka kuwasilisha kwake mpango mkakati endelevu wa usafi wa mazingira wilayani hapa utakaosaidia kuondoa adha ya mlundikano wa taka sehemu zisizo rasmi kwa muda mrefu.

Mwenyekiti wa soko hilo, Nafutari Joramu alieleza hofu ya kuibuka kwa mlipuko wa magonjwa licha ya kulipia ushuru wa uchafu kila mara.

Ofisa Usafi na Mazingira wilayani hapa, Budodi alisema suala la taka kukaa kwa muda mrefu limetokana na trekta iliyokuwa inatumika kuzoa taka kuwa na uchakavu wa matairi pamoja na mafuta hali iliyomkera Mkuu wa Wilaya.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Viviani Christiani, aliahidi kutekeleza agizo hilo la Mkuu wa Wilaya kwa kuondoa taka hizo na kuufanya Mji wa Maswa kuwa safi.

**Natoa saa mbili taka hizi ziondolewe hapa, suala la kusema trekta halina mafuta mara bovu sitaki kusikia, hivi wananchi wanatuelewaje?**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MAJI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan **akizindua moja ya mradi mkubwa wa majisafi unaohudumia wananchi.**

## MUHTASARI WA HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA MAJI 2024/2025

Mji wa Serikali, Mtaa wa Maji, S.L.P 456 Dodoma (barua@maji.go.tz)
+255 26 2322602/+255 26 2322602, Barua pepe, ps@maji.go.tz
www.maji.go.tz





# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI, MHE. JUMAA HAMIDU AWESO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA 2024/25

**Alhamisi ya tarehe 09 Mei, 2024, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), aliwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2024/2025. Ufuatao ni muhtasari wa Bajeti hiyo;**

## 1. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI

Naomba sasa kuelezea hali ya sekta ya maji nchini inayojumuisha rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; na huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini kama ifuatavyo:-

### 1.1 Hali ya Rasilimali za Maji na Ubora wa Maji

1. Nchi yetu inakadiriwa kuwa na rasilimali za maji zinazofaa kwa matumizi mbalimbali za wastani wa **mita za ujazo bilioni 126** kwa mwaka. Kiasi hicho kinahusisha maji juu ya ardhi **mita za ujazo bilioni 105** na maji chini ya ardhi **mita za ujazo bilioni 21**. Kwa idadi ya watu milioni 59.8 wa Tanzania Bara kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022, inaonesha kuwa kiasi cha maji kilichopo kwa mtu ni **mita za ujazo 2,105**. Kiasi hicho kipo juu ya kiwango cha chini cha mita za ujazo 1,700 cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa. Hali hiyo, inaonesha kuwa nchi yetu ipo juu ya kiwango cha uhaba wa maji *(water stress)*. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa vyanzo vya maji kiwango hicho kinaweza kupungua zaidi endapo hatua stahiki hazitachukuliwa.

   ***Taifa Letu lina usalama wa maji, lina maji mengi kwenye maziwa, mito, mabwawa na chini ya ardhi. Kazi yetu ni kuyafikisha maji hayo kwa wananchi.***

2. Ubora wa maji katika vyanzo vya maji hutofautiana kulingana na jiografia, tabianchi na mabadiliko ya tabianchi, shughuli za kibinadam na hali ya miamba. Takwimu zinaonesha hali ya ubora wa maji kwenye vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi inawezesha ustawi wa ikolojia na hivyo vinaweza kuendelezwa kwa matumizi ya sekta mbalimbali. Pamoja na hali hiyo ya ubora wa maji, bado kunahitajika jitihada za pamoja za kuzuia uchafuzi na pia, kurejesha na kuimarisha ubora wa maji katika vyanzo. Vilevile, maji yanayosambazwa vijijini na mijini yameendelea kukidhi viwango vya kitaifa vya ubora wa maji kwa matumizi ya kunywa na kupikia pamoja na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

### 1.2 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini

3. Upatikanaji wa huduma ya maji vijijini umefikia wastani wa **asilimia 79.6** mwezi Desemba, 2023 kutoka wastani wa **asilimia 77** mwezi Desemba, 2022. Ongezeko hilo limetokana na kutekelezwa kwa miradi ya maji **632** yenye vituo **7,956** vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi **4,740,959**. Hali hiyo, inafanya jumla ya wananchi wanaopata huduma ya maji kufikia **34,950,368** kati ya wananchi **39,232,999** wanaoishi maeneo ya vijijini. Dhamira ya Serikali ni kuona, zaidi ya **asilimia 85** ya wananchi wa vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2025.

   ***Ndugu zangu waheshimiwa wabunge wa majimbo ya vijijini kama Pangani, tunakoelekea tunahama kutoka kwenye vituo vya kuchotea maji na kuelekea kwenye kuunganisha maji katika kaya na majumbani, kwakuwa vijijini kuna nyumba nzuri zinazohitaji huduma hiyo. Wananchi wa vijijini nisikieni, endeleeni kujenga nyumba nzuri maji ya kuweka ndani yanakuja.***

### 1.1 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

4. Upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mijini umefikia wastani wa **asilimia 90** mwezi Desemba 2023 kutoka wastani wa **asilimia 88** mwezi Desemba, 2022. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi ya maji **85** inayohudumia wakazi **4,641,505** wa maeneo ya mijini. Dhamira ya Serikali ni kuona, zaidi ya **asilimia 95** ya wakazi wa mijini wanapata huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2025. Kwa upande wa huduma ya uondoshaji majitaka, mtandao unaotoa huduma hiyo nchini umefikia **kilomita 1,455.93** mwezi Aprili, 2024 na idadi ya wateja walioiunganishwa katika mtandao imefikia **58,650**. Kwa maeneo yasiyofikiwa na mtandao, huduma ya majitaka hutolewa na magari maalum ambayo huyakusanya na kutibiwa kwenye mabwawa ya kutibu majitaka.

   ***Kwa mwenendo huu, kwa uongozi mahiri wa Mama Samia na kwa ushirikiano mkubwa wa Bunge lako na ufuatiliaji wa Waheshimiwa Wabunge, Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 iliyotuelekeza kufikia zaidi ya asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini inatekelezwa barabara. Narudia, Ilani ya Chama Tawala inatekelezeka barabara. CCM ndiyo mwenye duka, sisi shopkeepers, tutatimiza wajibu wetu mchana na usiku, iwe mvua, liwe jua na kwenye mabonde na milima.***

## 2. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

### 2.1 Upatikanaji wa Fedha

5. Katika mwaka 2023/24, Fungu 49 – Wizara ya Maji liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 756.2**, ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 60.3** ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi Bilioni 695.8** ni fedha za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, **Shilingi Bilioni 407.1** ni fedha za ndani na **Shilingi** Bilioni **288.7** ni fedha za nje. Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi Bilioni 42.3** ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji na **Shilingi Bilioni 18.0** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

6. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 638.7,** sawa na **asilimia 84.5** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 593.4** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo **Shilingi Bilioni 356.9** sawa na **asilimia 87** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni 236.5** sawa na **asilimia 81.9** ni fedha za nje. Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, jumla ya **Shilingi Bilioni 45.3** zimetolewa, ambapo **Shilingi Bilioni 36.5** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi Bilioni 8.8** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

### 2.1 Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo

Utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2023/24 umeainishwa katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; huduma za usambazaji majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini; na kazi mbalimbali zinazotekelezwa katika taasisi chini ya Wizara pamoja na masuala mtambuka.

### 2.0.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

7. Usimamizi wa rasilimali za maji unahusisha ujenzi na ukarabati wa vituo vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji, udhibiti wa matumizi ya maji na migogoro, ujenzi na usajili wa mabwawa, udhibiti wa uchimbaji wa visima, ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji na kuzuia uchafuzi wa vyanzo.

***Usimamizi wa rasilimali za maji ni sayansi na vilevile ni suala la kijamii. Sisi Wizara ya Maji tumejifunza kuwa jamii siku zote ipo na iko tayari na inaposhirikishwa kuna mafanikio makubwa. Ninyi Waheshimiwa Wabunge ndio wawakilishi wa jamii na hivyo Wizara itaendelea kuwashirikisha katika usimamizi wa rasilimali za maji na tunaomba iwe moja ya agenda yenu kuu majimboni. Sauti ya Mbunge ni kubwa. Tufikishieni shukrani zetu wa wananchi wenu.***

### 2.0.1 Ubora wa Maji

8. Wizara imeendelea kuhakikisha maji yanayosambazwa vijijini na mijini yanakidhi viwango vya kitaifa vya ubora wa maji kwa matumizi ya kunywa na kupikia pamoja na shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na uhakiki wa ubora wa maji kwenye **vyanzo 1,625**. Aidha, Wizara inaendelea kuhakiki ubora wa madawa yanayotumika kutibu na kusafisha maji; kufuatilia ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira; na kuziimarisha maabara za ubora wa maji.

   ***Falsafa yetu ni falsafa ya afya, kuwa unanawa kabla ya kula. Hivyo, Wizara yetu inahakikisha wananchi wanakunywa maji yenye ubora unaokubalika Kitaifa na Kimataifa na wananawiri. Afya ndio mtaji wa kila kitu.***

### 2.0.1 Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

9. Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kwa kujenga, kukarabati, kupanua mitandao ya kusambaza maji; na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji. Katika mwaka 2023/24, Serikali ilipanga kutekeleza jumla ya miradi **1,546** katika maeneo mbalimbali ya vijijini. Hadi mwezi Aprili, 2024, jumla ya miradi **632** yenye vituo **7,956** imetekelezwa na kutoa huduma kwa wananchi wapatao **4,740,959**. Aidha, utekelezaji wa miradi ya maji **872** vijijini unaendelea na upo katika hatua mbalimbali. Baadhi ya miradi mikubwa ya maji vijijini inayoendelea na utekelezaji ni pamoja na miradi ya maji ya Ruangwa, Lindi na Nachingwea; Mkinga – Horohoro; Diburuma – Songe; Morong'anya - Morogoro Vijijini; Monduli; Ukiliguru, Sumve hadi Koromije; na Ilujamate – Buhingo.

10. Katika kuongeza kasi ya uendelezaji wa rasilimali za maji na utekelezaji wa miradi ya maji, Serikali ilinunua mitambo 25 ya uchimbaji visima na seti 5 za mitambo ya ujenzi wa mabwawa. Mwongozo wa matumizi ya mitambo hiyo umetolewa ili itumike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa. Katika mwaka 2023/24, Serikali kupitia mitambo hiyo imechimba visima **266** kwenye maeneo mbalimbali ya vijijini. Vilevile, Serikali imefanya tathimini na kuandaa mpango wa kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji ambavyo havina huduma ya maji ambapo jumla visima **900** vinatarajiwa kuchimbwa katika majimbo mbalimbali ya uchaguzi. Hadi sasa kazi ya uchimbaji visima imeanza katika mikoa ya Kigoma, Manyara na Songwe na utafiti unaendelea kwenye mikoa mingine.

11.

***Kila jimbo la kijijini litachimbiwa visima. Narudia, kila Jimbo la vijijini litachimbiwa visima. Narudia tena, kila Jimbo la Vijijini litachimbiwa visima na asiyepata kisima atapata bwawa. Wali wa kushiba, unaonekana kwenye sahani. Huu wali unatosha na tunasaza.***

12. Serikali inaendelea na ujenzi wa mabwawa ya ukubwa wa kati na madogo katika maeneo mbalimbali hususan maeneo kame. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imekamilisha ujenzi na ukarabati wa mabwawa **14** na inaendelea na ujenzi wa mabwawa **25**. Mabwawa yaliyokamilika ni Uhelera na Bahimakuru katika Wilaya ya Bahi; Igumangobo na Ilambambasa (Maswa); Ng'walukwa (Shinyanga); Ngofila (Kishapu); Qang'dend (Karatu); na Horohoro na Mbuta (Mkinga); Chole (Kisarawe); Kwamaizi (Handeni); Makame (Kiteto), Enguikumet II (Monduli) na bwawa la Mwadila Wilayani Maswa. Aidha, Serikali imeendelea kuzihamasisha taasisi za kijamii, asasi na watu binafsi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya majengo. Pia, Serikali imejenga matanki ya mfano kwenye maeneo ya shule, zahanati na masoko katika Halmashauri mbalimbali nchini.

*Kazi ya mitambo ya kujenga mabwawa ya Mama Samia imejidhihirisha katika Majimbo ya Bahi, Maswa, Kishapu, Karatu, Mkinga, Kisarawe, Handeni, Kiteto na Monduli na kwingineko kwa kuchimba mabwawa kwa kutumia wataalam wa Wizara. Kazi hii inaendelea na ndio kwanza kunakucha kama ni mkoko ndio unaanika maua*

13. Katika kuhakikisha uendelevu wa huduma ya maji vijijini, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza programu na miradi ifuatayo:-

**(a) Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

14. Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza Programu ya Malipo kwa Matokeo (PforR) kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 350.** Awali utekelezaji wa Programu hiyo umefanyika katika Halmashauri za Wilaya **86** kwenye mikoa **17**. Kupitia programu hiyo, jumla ya miradi **540** katika vijiji **1,118** imetekelezwa inayonufaisha wananchi wapatao **milioni 4.1**. Matokeo hayo, yamevuka lengo la awali la kunufaisha wananchi **milioni 3** na hivyo, katika Mkutano wa Mawaziri wa Maji na Fedha wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika uliofanyika Addis Ababa nchini Ethiopia mwezi Novemba 2023, Benki ya Dunia iliitambua Tanzania kuwa kinara katika utekelezaji wa Programu hiyo. Kutokana na mafanikio hayo, Tanzania imeongezewa fedha za Programu kutoka **Dola za Marekani milioni 350** hadi **milioni 654** na kuongeza mikoa inayonufaika kutoka **17** hadi **25** na Halmashauri kutoka **86** hadi **137**.

***Kwa mara mbili mfululizo, Tanzania imealikwa na Benki ya Dunia kutoa ushuhuda na uzoefu wa kuwa kinara wa PforR Duniani. Hii, imefanyika mwezi Machi, 2023 Jijini New York – Marekani, wakati wa mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Maji. Vilevile, imefanyika Novemba, 2023 Addis Ababa – Ethiopia wakati wa Mkutano wa Mawaziri wa Maji na Fedha wa Kanda za Mashariki na Kusini mwa Afrika.***

***Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Daktari Victoria Kwakwa ameipongeza Tanzania kwa kuwa kinara wa kutekeleza PforR Duniani. Narudia, katika nchi zaidi ya 50 katika Mabara Matatu, Tanzania ndio kinara wa PforR Duniani. Narudia tena, Tanzania ndio nambari one, katika kutekeleza PforR Duniani. Mama Samia anaupiga mwingi sana hadi unamwagika.***

***Sasa PforR iko mikoa 25 na Halmashauri za Wilaya 137. PforR inang'arisha vijiji vya Tanzania.***

**(b) Uimarishaji wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (*CBWSOs*)**

15. Wizara imeendelea kuunda, kusajili, kuunganisha na kuvijengea uwezo Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii *(CBWSOs)*. Hadi mwezi Aprili, 2024, uundaji na usajili wa CBWSOs **100** na uunganishaji wa CBWSOs **517** ulikuwa umekamilika na hivyo, kufanya jumla ya CBWSOs zilizosajiliwa kufikia **1,382**. Vyombo hivyo vimetoa fursa za ajira kwa vijana **5,342** katika kada za ufundi, uhasibu na saidizi.

***CBWSOs zinachangia kupunguza tatizo la ajira nchini, na zinaimarisha huduma za maji vijijini. Maji ni maisha na maji ni ajira. Zizi lisilo na ndama limekufa, CBWSOs ni chombo cha kuandaa na kukuza wafanyakazi wa Sekta ya Maji wa leo na kesho.***

**2.0.1. Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

16. Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini. Katika mwaka 2023/24, jumla ya miradi **244** ilipangwa kutekelezwa ambapo hadi mwezi Aprili 2024, miradi **85** imekamilika na miradi **159** ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo, na Miradi ya Kitaifa ni kama ifuatavyo: -

17. Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maji na usafi wa mazingira mijini ni kama ifuatavyo:-

**(a) Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha**

18. Wizara imekamilisha utekelezaji wa mradi wa majisafi na usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 233.9**. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 40** hadi **lita milioni 200** kwa siku hivyo, kukidhi mahitaji ya maji kwa Jiji la Arusha; kuongeza huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka **asilimia 7.6** hadi **30**; na kupunguza upotevu wa maji kutoka **asilimia 48** hadi **39**. Kazi iliyobaki ni kuendelea na usambazaji katika maeneo ya Kiseriani, Sekeleni, Moivalo, Shangarai, Maweni, Karangai, Msitu wa Mbogo, Shambarai Burka, Matiba, Valeska, Patanumbe, Kinyaki, Siwandeti, Tarakwa na Kata ya Kiutu.

***Huduma ya maji katika Jiji la Arusha ni ya uhakika na hivyo inalinda na kulipa hadhi Jiji la Arusha ambalo ni kitovu cha utalii nchini. Huduma ya Maji Arusha inapeperusha agenda ya Royal Tour, Agenda ya Mheshimiwa Rais Mama Samia.***

**(b) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na Baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Pwani**

19. Wizara inatekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na miji ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo mkoani Pwani. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa kipande cha kwanza na cha pili cha mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka visima virefu vya Kimbiji kwa gharama ya **Shilingi bilioni 21.28** umekamilika na kunufaisha wakazi **250,000** wa Chanika, Luzando, Mpera, Chamazi, Kitunda, Kinyerezi, Temeke, Kisarawe, Kibada, Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Keko na Chang'ombe. Vilevile, kipande cha tatu cha mradi wa ujenzi wa mtandao wa mabomba ya maji wa Kimbiji – Kigamboni utekelezaji umefikia **asilimia 75** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kwa upande wa Kibamba maeneo yatakayonufaika ni pamoja na Msakuzi, Makabe, Msumi A, Msumi B, Msumi C, Mpiji Magoe na Tegeta A.

20. Wizara imeanza kujenga mtandao wa usambazaji maji na matanki ya kuhifadhi maji Kusini mwa Dar es Salaam kwa gharama ya **Shilingi bilioni 35.15**. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 19** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kunufaisha wakazi wapatao **450,000** wa maeneo ya Bangulo, Mwanagati, Kitunda, Kipunguni, Majohe, Kivule, Magole, Msongola, Chanika na Chalambe. Aidha, Wizara inatekeleza mradi wa usambazaji majisafi maeneo yaliyo nje ya mtandao kwa gharama ya **Shilingi bilioni 22.08**. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji umefikia **asilimia 96** na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei 2024 na kunufaisha wakazi **215,380** wa maeneo ya Kisewe, Magengeni, Dovya, Mwembebamia, Mianzini, Mwanamtoti, Butiama, Mgeule, Mgeule Juu, Upendo, Tungi, Magogoni, Ferry, Nzasa A, Somelo, Kifurukwe, Kichangani, Yangeyange na Vumba yaliyopo Kigamboni, Temeke na Ilala.

***Dar es Salaam ni Jiji kubwa, Jiji la kibiashara na mboni ya Taifa, hekaheka zake ni kama sherehe za Krismasi au Eid. Hivyo Wizara iko macho na huduma za maji Dar es Salaam. Waheshimiwa wa Majimbo yanayohudumiwa na DAWASA asanteni sana kwa ushirikiano wenu.***

21. Vilevile, Serikali inaendelea kujenga bwawa la kimkakati la Kidunda litakalohudumia Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Mkoa wa Pwani na Morogoro Vijijini ambapo ujenzi umefikia **asilimia 18**.

***Wazo la ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni la miaka na miaka, tangu miaka ya 1950. Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere amelikuta na ameliendeleza. Baada ya miaka zaidi ya 60, Mama Samia anajenga Bwawa la Kidunda tena kwa fedha za ndani. Chezea Mama Samia wewe, hakika hii inadhihirisha umuhimu wa kipindi cha TV cha Songa na Samia cha Zuhura Yunus. Songa na Samia, Songa na Samia, Songa na Samia.***

***Bwawa hili ni muarobaini wa shida ya maji katika Majimbo ya Chalinze, Bagamoyo, Kibamba, Ubungo, Kawe, Kinondoni, Ilala, Kigamboni, Segerea, Ukonga, Kisarawe, Mkuranga, Mbagala, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini, na sehemu za Handeni na Morogoro Vijijini. Waheshimiwa Wabunge, mambo yako bambam, bambam, bambam sana.***

**(c) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dodoma**

22. Wizara imeendelea kutekeleza mipango ya muda mfupi inayolenga kukabiliana na adha ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma ambapo hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imekamilisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi na uboreshaji wa mtandao wa majisafi Nzuguni unaohudumia wakazi **75,968** wa maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Kisasa. Aidha, awamu ya pili ya mradi imeanza kwa gharama ya **Shilingi bilioni 5.51** na utanufaisha wakazi wapatao **80,000**. Vilevile, utekelezaji wa mradi wa kupanua na kuboresha huduma ya majisafi Dodoma na Chamwino unaogharimu **Shilingi bilioni 4.18** unaendelea na umefikia **asilimia 40** na unatarajia kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kunufaisha wakazi **150,000** wa Dodoma na Chamwino.

23. Serikali inaendelea taratibu za maandalizi za ujenzi wa Bwawa la Kimkakati la la Farkwa litakalohudumia Jiji la Dodoma na wilaya za Chemba, Chamwino na Bahi. Kazi inayoendelea ni mapitio ya usanifu wa bwawa pamoja na uandaaji wa mpango wa kulinda na kutunza mazingira katika vyanzo vya maji vitakavyopeleka maji kwenye bwawa. Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2024/25.

**(d) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mwanza na Maeneo ya Pembezoni**

24. Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa chujio la Butimba kwa gharama ya takriban **Shilingi bilioni 80.19**. Mradi huo ulihusisha Kukamilika kwa mradi huo, kumeboresha huduma ya maji kwa wakazi wapatao **450,000** katika Jiji la Mwanza. Maeneo yanayonufaika na mradi huu ni pamoja na Nyegezi, Luchelele, Kishiri, Igoma, Nyamhongolo katika Jimbo la Nyamagana. Aidha, kazi iliyobaki ni ujenzi wa matanki matano (5) yatakayosambaza maji katika maeneo ya Fumagila, Nyamazobe, Usagara, Kisesa na Buhongwa.

25. Vilevile, utekelezaji wa mradi wa kupanua mtandao wa usambazaji maji katika Miji ya Magu na Misungwi unaogharimu **Shilingi bilioni 1.94** unaendelea na hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji umefikia **asilimia 70** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Pia, utekelezaji wa mradi wa kuboresha mfumo wa usambazaji maji katika Jiji la Mwanza unaogharimu **Shilingi bilioni 4.62** umefikia **asilimia 70** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kunufaisha wakazi wapatao **33,000**.

***Kanda ya Ziwa yote, Mungu amewapendelea kwa kuwapa Ziwa Victoria. Wizara inahakikisha mnapata majisafi, salama na ya kutosheleza kutoka Ziwa Victoria. Wahenga walisema, kula uhondo kwataka matendo, pasi matendo utakula uvundo. Mradi wa Butimba umedhihirisha kuwa, kwa nia njema na juhudi za Mama Samia, Mwanza sasa mnaendelea kula uhondo.***

**(e) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mbeya**

26. Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Jiji la Mbeya kwa kutumia chanzo cha Mto Kiwira unaogharimu **Shilingi bilioni 99.66**. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 66.5** hadi **lita milioni 184** kwa siku. Hadi mwezi Aprili 2024, ujenzi wa banio na tanki la maji lenye ujazo wa **lita milioni 5** ulikuwa umefikia **asilimia 11**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2025 na kunufaisha wakazi **milioni 1.45** wa Jiji la Mbeya, Mji wa Mbalizi na Vijiji vya Ngumburu, Mbei 1, Swaya Juu na Malangali. Vilevile, Wizara inatekeleza kipande cha kwanza na cha pili cha mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Kata za Mwansekwa na Iganzo kwa gharama ya **Shilingi**





**bilioni 5.2**. Utekelezaji katika Kipande cha kwanza umefikia **asilimia 90** na kipande cha pili **asilimia 76**. Mradi umeanza kuzalisha maji **lita milioni 2** kwa siku na umeanza kutoa huduma kwa wananchi.

***Mheshimiwa Spika, kwa majukumu makubwa uliyonayo ya kuongoza muhimili wa Bunge na kuwa Rais wa IPU Duniani, unahitaji utulivu mkubwa ili kutekeleza majukumu hayo ya Kitaifa na Kimataifa. Mradi wa Kiwira na Shughuli nyingine za maji mkoani Mbeya zinalenga kukupa wewe na Wabunge wote wana maji ya kutosha wakati wote.***

**(f) Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari – Butiama**

27. Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia *(Saudi Fund for Development – SFD)* inatekeleza mradi wa maji Mugango, Kiabakari na Butiama kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.69**. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 98.7** na umeanza kutoa huduma na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2024. Mradi utawanufaisha zaidi ya wananchi **100,000** waliopo katika eneo la mradi; na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka bomba kuu. Aidha, wananchi wa Kata ya Nyamswa yenye vijiji vya Nyamswa, Makongoro A, Makongoro B na Bukama watanufaika na upanuzi wa mradi huo.

***Mradi huu ni fahari kubwa ya kuendelea kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kupitia upatikanaji wa maji katika Kijiji cha Butiama na Wilaya ya Butiama kwa ujumla na Jimboni kwa Profesa mashuhuri Sospeter Mhongo.***

**(g) Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe**

28. Wizara kwa kushirikiana na BADEA, OPEC Fund na Kuwait Fund inatekeleza mradi wa maji Same – Mwanga - Korogwe utakaohudumia Miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji **38** vya Wilaya za Same na Mwanga na vijiji vitano (**5**) vya Wilaya ya Korogwe. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 86.7** na kwa sasa upo kwenye majaribio ya kutoa maji kutoka katika chanzo kuyapeleka kwenye chujio. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi **456,931** wa wilaya za Same, Mwanga na Korogwe.

***Naomba Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo ya Mwanga, Same Magharibi, Same Mashariki na Korogwe Vijijini muendelee kuungana na Wizara katika kusoma Wakorinto wa Pili 6:2 inayosema, "Wakati uliokubalika nalikusikia, siku ya wokovu nalikusaidia; Tazama, Wakati uliokubalika ndio sasa; Tazama, Siku ya Wokovu ndio sasa." Wakati wa maji ya Same Mwanga ndio huu. Mama Samia anaweka Historia Same na Mwanga.***

**(h) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28**

29. Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ambapo miji 24 inatekelezwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim - India na miji minne (4) inatekelezwa kwa fedha za ndani. Kwa mujibu wa Mkataba, mradi huo wa miji 28 unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26 na utanufaisha wananchi katika Miji ya Handeni, Muheza, Pangani, Korogwe, Kilwa Masoko, Nanyumbu, Ifakara, Rujewa, Makambako, Wanging'ombe, Njombe, Chunya, Chamwino, Chemba, Manyoni, Singida, Kiomboi, Mugumu, Kaliua, Urambo, Sikonge, Kasulu, Mpanda, Geita, Chato, Kayanga, Mafinga, Makonde, Songea, Rorya na Tarime.
30. Hatua za utekelezaji wa mradi ni kama zinazvyoonekana katika Hotuba yangu Ukurasa wa 70.

***Waheshimiwa Wabunge, Mradi wa Miji 28 ni wenu, tunaomba muendelee kuusimamia na Wizara itaendelea kuwashirikisha katika hatua zote za kutekeleza mradi huu. Anaelala na mgonjwa ndie anaejua mihemo yake, nyinyi Waheshimiwa Wabunge ndio mko na mgonjwa. Mnaujua Mradi wa Miji 28. Tushirikiane. Lazima katika kila mji na mradi wote, tupate point tatu (3) na magoli kibao.***

**(i) Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu**

31. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)* na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Green Climate Fund - GCF)* kwa gharama ya **Shilingi bilioni 444.6.** Mradi huo unatekelezwa kwenye Wilaya tano (5) za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu katika Mkoa wa Simiyu na unahusisha usanifu na ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji, uhifadhi na usambazaji wa maji katika wilaya hizo. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zinazoendelea ni ujenzi wa matanki ya maji **sita (6)** yenye jumla ya ujazo wa **lita milioni 39.5**; upimaji na uhakiki wa njia kuu ya kulaza mabomba. Kwa wastani utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 4 na unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2026 na kunufaisha wananchi wapatao **662,500** kwenye wilaya hizo.

***Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo ya Maswa Mashariki, Maswa Magharibi, Kisesa, Meatu, Bariadi, Itilima na Busega; mkiona vinaelea, vimeundwa. Ninyi ndio waundaji wa mradi wa Simiyu.***

**2.0.2. Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji (*National Water Master Plan*)**

32. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza kuandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji katika mikoa ya Rukwa, Dodoma na Njombe na zoezi hilo litaendelea katika mikoa mingine iliyobakia katika mwaka 2024/25.

**2.0.3. Gridi ya Taifa ya Maji**

33. Wizara inaendelea na maandalizi ya Gridi ya Taifa ya Maji na kwa sasa hatua iliyofikiwa ni ya kuajiri Mtaalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa mpango huo. Aidha, Wizara imeanza kutumia vyanzo vikubwa vya maji vya uhakika ikiwemo maziwa, mito mikubwa na mabwawa kwa ajili ya kusambaza huduma ya maji kwenye maeneo ambayo hayana vyanzo vya uhakika vya maji. Kwa mfano; mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria ambao umenufaisha Miji ya Kahama, Shinyanga, Tinde, Nzega, Tabora, Igunga na Shelui. Vilevile, taratibu za manunuzi za kumpata mtaalam mshauri wa kutoa maji Ziwa Tanganyika na kuyapeleka katika mikoa ya Katavi, Rukwa mpaka Kigoma zimeanza. Pia, Wizara imesaini Mkataba na Mtaalam Mshauri atakaefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyapeleka Dodoma.

***Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo yaliyo katika mwambao wa Maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria pamoja na maeneo kame, mtoto wenu National Water Grid karibu anazaliwa. Maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria yana asilimia 25 ya maji yote matamu duniani, hivyo maono hayo makubwa ya Mama Samia lazima tuyatekeleze. Na sisi Wizara ya Maji, hatutakuwa kikwazo. Narudia, Mradi wa National Water Grid ni maono makubwa ya Taifa linalojiamini na kuthubutu. Taifa hilo ni Tanzania chini ya Mama Samia.***

**2.0.4. Matumizi ya Dira za Maji za Malipo Kabla**

34. Wizara imeanza kutumia teknolojia ya matumizi ya dira za maji za malipo kabla *(pre-paid water meters)* kwa lengo la kupunguza maji yanayopotea na malalamiko yanayohusiana na ankara za maji. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya wateja **13,526** katika maeneo ya vijijini na mijini wamefungiwa dira hizo zikiwemo Mamlaka za Maji za Iringa ambayo imefunga dira **6,544**, Dodoma **(1,085)** na Mamlaka ya Maji Tanga **dira 627**. Kwa upande wa vijijini, RUWASA imewafungia dira hizo wateja **1,846** kwenye mikoa mbalimbali.

35. Mnamo tarehe 4 Machi, 2024, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** aliielekeza Wizara ya Maji kuongeza kasi ya ufungaji wa Dira za maji za malipo kabla ili kuwafikia wananchi wote nchini. Katika kutekeleza agizo hilo, Wizara imeandaa Mkakati wa Kuongeza Kasi ya Ufungaji wa Dira za Maji za Malipo Kabla ambapo kupitia Mkakati huo asilimia 50 ya wateja wa maji vijijini na mijini watafungiwa dira hizo ifikapo Desemba 2025.

***Hili ni agizo la Mama Samia kwa Wizara ya Maji. Nasi tunamhakikishia Mama kupitia Ezra 10:4 kuwa kazi tunaiweza na timu ya Wizara iko imara kuitenda kwa uaminifu. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuhamasishe wananchi kufunga Dira za malipo kabla ya matumizi. Hizi ni LUKU za maji. Hii ndio Dunia ya kisasa na huu ndio mwelekeo. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais, kuwa lugha yetu ni pre - paid meters, na maono yetu ni kuwa na viwanda vya pre paid meters***

**3. MAFANIKIO YA SEKTA YA MAJI KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

36. Katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** sekta ya maji imepata mafanikio makubwa yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa **asilimia 77** mwezi Desemba, 2022 hadi **asilimia 79.6** mwezi Desemba**,** 2023 na mijini kutoka wastani wa **asilimia 88** mwezi Desemba, 2022 hadi **asilimia 90** mwezi Desemba, 2023;
(ii) Kupatikana kwa chanzo kipya cha fedha za utekelezaji wa miradi ya maji kupitia Hati Fungani ambapo Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga imekuwa ya kwanza kuzindua uuzaji wa Hati Fungani ya Kijani yenye thamani ya **Shilingi bilioni 53.12**;

***Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga imekuwa Taasisi ya kwanza Tanzania na Afrika Mashariki kuingia katika Soko la Hisa na imepata fedha Shilingi Bilioni 54.72 sawa na asilimia 103. Narudia, imevunja rekodi ya kuwa Taasisi ya kwanza Tanzania na Afrika Mashariki. Huu ni ubunifu na udhubutu mkubwa. Tunawashukuru Watanzania na Waheshimiwa Wabunge kwa kununua hisa za Mamlaka ya Maji Tanga. Hili ni funzo kuwa, It can be done, play your part.***

(iii) Kufikiwa kwa malengo ya programu ya *PforR* kwa muda uliopangwa, hivyo Benki ya Dunia kuitambua Tanzania kuwa nchi ya kwanza kufanya vizuri kati ya nchi zaidi ya 50 duniani zinazotekeleza Programu hiyo kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo;
(iv)
(v) Kukamilika kwa miradi mikubwa na ya kimkakati ikiwemo mradi wa maji Arusha; Butimba; Mugango Kiabakari – Butiama; na Bunda;
(vi)
(vii) Kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa kuwa na Gridi ya Taifa ya Maji kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji ikiwemo maziwa, mito na mabwawa kupeleka maji maeneo yasiyo na vyanzo vya uhakika;

(viii) Kuanza kwa utekelezaji wa miradi ya maji ya kimkakati ikiwemo mabwawa ya Kidunda na Farkwa pamoja na miradi ya Miji 28, Kiwira, Ruangwa na Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi – Simiyu; Kuanzishwa kwa *Consultancy Bureau* katika Chuo cha Maji inayosaidia kutoa huduma za ushauri elekezi kwenye sekta ya maji na sekta nyingine;

(ix) Kuendelea kukwamua miradi ya maji vijijini iliyokuwa na changamoto ya kutokukamilika kwa muda mrefu ambapo miradi **164** kati ya miradi **177** imekwamuliwa;

(x) Kuimarika kwa mazingira ya kazi kutokana na kukamilika na kuanza

kutumika kwa jengo jipya la ofisi za Wizara lililopo Mtumba pamoja na ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo **magari 124**, **pikipiki 191** na **kompyuta 95**;

(xi) Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa mabwawa **14** ya ukubwa wa kati na madogo ya kuvuna maji ya mvua kwenye maeneo mbalimbali nchini yenye uwezo wa kuhifadhi maji **lita bilioni 1.86**;

(xii) Kuongezeka kwa ufanisi katika uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa kwa kutumia mitambo iliyonunuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambapo jumla ya **visima 283** vimechimbwa. Aidha, mitambo hiyo imesaidia kukabiliana na janga la maafa la Hanang' mkoani Manyara kwa kuchimba visima **nane (8)** na kukarabati Bwawa la Nanja; na kuchimba visima **sita (6)** vinavyohudumia wananchi katika eneo la Msomera;

(xiii) Kuimarika kwa ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maji ambapo kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo miradi ya maji imekuwa ikifanya vizuri (*clean sheet*) katika Mbio za Mwenge wa Uhuru;

(xiv) Kuwezesha CBWSOs kujiunga kwenye mfumo wa makusanyo ya fedha za umma *(GePG)* na hivyo kurahisisha usimamizi wa mapato yao; na

(xv) Kuimarika kwa ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo wenye nia ya kuwekeza katika Sekta ya Maji wakiwemo Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), CSOs , NGOs, KfW.

## 4. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

37. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24, Wizara imekabiliana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni uchafuzi, uharibifu na uvamizi wa vyanzo vya maji; mahitaji makubwa ya fedha za uwekezaji kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maji; na mabadiliko ya tabianchi.

38. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuimarisha usimamizi na uendelevu wa rasilimali za maji; uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa kuviwekea mipaka na kuvitangaza kwenye gazeti la Serikali; kutoa elimu kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa rasilimali za maji; kuendelea kufanya mazungumzo na wadau mbalimbali ili kupata fedha za kutekeleza miradi; na kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa lengo la kuhifadhi maji na kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

*Maelezo ya kina kuhusu changamoto na hatua za kukabiliana nazo yanapatikana ukurasa wa 105 hadi 108 wa kitabu cha hotuba yangu*

## 5. VIPAUMBELE NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

39. Wizara imeweka vipaumbele ambavyo vitazingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka 2024/25 ili kufikia lengo la kuwapatia huduma ya maji safi na salama kwa zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wa vijijini na zaidi ya asilimia 95 ya wakazi wa mijini. Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji;

(ii) Kukamilisha utekelezaji wa miradi inayoendelea na kuendelea na ujenzi wa miradi mikubwa;

(iii) Kuendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza kasi ya uvunaji wa maji ya mvua kupitia ujenzi wa mabwawa ya ukubwa wa kati na mabwawa ya kimkakati kwa kushirikiana na Sekta za Mifugo, Kilimo, Utalii na Mazingira;

(iv) Kuimarisha matumizi ya mitambo ya uchimbaji wa visima na mabwawa iliyonunuliwa ili kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji ambavyo havina huduma ikiwa ni pamoja na kutekeleza Programu ya kuchimba visima 900 na ujenzi wa mabwawa madogo madogo;

(v) Kukamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji *(Water Master Plan),* Mtandao wa Taifa wa Kusambaza Maji *(National Water Grid)* na kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002;

(vi) Kupunguza upotevu wa maji kwa kuendelea kukarabati miundombinu chakavu, kufunga mifumo ya kuweza kutambua maeneo yenye mivujo (ILMS) na kushirikisha viongozi wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutoa taarifa za upotevu wa maji kwa wakati;

(vii) Kuongeza kasi ya ufungaji wa dira za malipo kabla ya matumizi ya maji *(prepaid meters)* ili kuongeza makusanyo na kupunguza malalamiko ya wateja;

(viii) Kuongeza kasi ya uwekezaji wa miundombinu ya uondoshaji majitaka kwenye Miji Mikuu ya Mikoa na Wilaya;

(ix) Kuimarisha utoaji wa huduma bora ya majisafi kupitia Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira na CBWSOs kwenye eneo la maunganisho ya wateja wapya na kuhakikisha masaa ya upatikanaji wa huduma ya maji yanaongezeka; na

(x) Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na uendeshaji wa miradi na skimu za maji.

40. Mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25 umezingatia vipaumbele nilivyovitajwa hapo juu pamoja na masuala ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; usimamizi wa huduma za ubora wa maji; huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini; na kujenga uwezo wa Wizara na taasisi zake.

### 5.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

#### 5.1.1 Usimamizi wa Rasilimali za Maji

41. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa rasilimali za maji kwa kukarabati vituo **100** vya usimamizi wa rasilimali za maji; kutoa vibali **600** vya matumizi ya maji; kuunda jumuiya **18** za watumia maji; na kuunda kamati **30** za vidakio vya maji. Pia, Wizara itaendelea kutambua, kuimarisha ulinzi, uhifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji.

#### 5.1.1 Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

42. Uendelezaji wa rasilimali za maji unahusisha kazi za utafutaji na uendelezaji wa vyanzo vya maji chini na juu ya ardhi pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua. Kwa upande wa uvunaji wa maji ya mvua, Serikali inaendelea kujenga mabwawa ya kimkakati, mabwawa ya kati na madogo. pamoja na uandaaji wa mpango wa kulinda na kutunza mazingira katika vyanzo vya maji vitakavyopeleka maji kwenye mabwawa. Suala la mabadiliko ya tabianchi yanaleta athari ya ukame na mafuriko hivyo, katika mwaka 2024/25, Serikali imepanga kuendelea na ujenzi wa bwawa la kimkakati la Kidunda na kuanza mradi wa ujenzi wa bwawa la Farkwa; kukarabati mabwawa **19** na kuendelea na ujenzi wa mabwawa **25** ya ukubwa wa kati na mdogo; na kufanya usanifu wa mabwawa **45.**

### 5.2 Usimamizi wa Huduma ya Ubora wa Maji

43. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kufanya tathmini na ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji **2,200**, mifumo ya usambazaji maji **8,245** vijijini na mijini, na mifumo **150** ya majitaka. Vilevile, Wizara itaendelea kuziboresha maabara za maji kwa kuzipatia vitendea kazi na kuziwezesha kupata na kudumisha hadhi ya ithibati katika viwango vya kimataifa.

### 5.2 Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

44. Katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kuendelea kutekeleza jumla ya miradi **1,054** ya usambazaji maji vijijini katika maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo yanayozunguka vyanzo vya Bwawa la Kidunda na vijiji vilivyopitiwa na mradi wa Same Mwanga. Aidha, kuendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya maji, kuzijengea uwezo *CBWSOs* ili kuimarisha uwezo wa kujiendesha.

### 5.2. Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

45. Katika mwaka 2024/25, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo pamoja na sekta binafsi imepanga kutekeleza jumla ya miradi **245** ya maji kwenye maeneo ya mijini ikiwemo mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kwenda Mtwara; mradi wa kutoa maji Mto Momba kwenda Tunduma; na kutoa maji kutoka tanki la Bisarye kwenda Nyamuswa na kuanza usanifu wa mradi wa kutoa maji Mto Rufiji kwenda Lindi. Aidha, Wizara imepanga kuendelea na ujenzi wa miradi ya uondoshaji wa majitaka katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya na miji midogo.

**5.3.** Kwa upande wa Jiji la Dodoma, Wizara itaanza ujenzi wa mradi wa bwawa la Farkwa; na mpango wa muda mrefu ni kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Jiji la Dodoma kupitia Singida.

5.6 Wizara imejipanga kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya mijini kwa kuhakikisha maunganisho kwa wateja yanafanyika ndani ya siku saba, mwananchi ana haki ya kutokatiwa huduma ya maji kwa siku za mapumziko ya mwisho wa wiki na siku za sikukuu. Aidha, Wizara itahakikisha suala la kupambana na upotevu wa maji linafanyika kikamilifu na Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji watapimwa kwa kiwango kinachopotea na Mkurugenzi atakayeshindwa kudhibiti suala hili hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yake.

### 5.4 Kujenga Uwezo wa Kitaasisi

46. Katika mwaka 2024/25, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002; kuendelea kujenga uwezo wa kitaasisi wa sekta ya maji ikiwa ni pamoja na watumishi na kukiwezesha Chuo cha Maji kuendelea kutoa wataalam kulingana na mahitaji. Aidha, Wizara itaendelea kuujengea uwezo Mfuko wa Taifa wa Maji ili uweze kupata ithibati kwa ajili ya kupata fedha za Mifuko ya Mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA; na ufuatiliaji na tathmini ili kuongeza ufanisi.

## 6. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25

47. Ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 627,778,338,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/25, ambapo **Shilingi 69,662,959,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 558,115,379,000** ni fedha za maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 17,542,812,000** ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo (*OC*) na **Shilingi 52,120,147,000** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (*PE*) ya watumishi wa Wizara, RUWASA, Mfuko wa Taifa wa Maji na Chuo cha Maji. Kwa upande wa fedha za maendeleo, **Shilingi 340,463,656,000** sawa na **asilimia 61** ni fedha za ndani na **Shilingi 217,651,723,000** sawa na **asilimia 39** ni fedha za nje.

**Hotuba inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Maji yenye kikoa cha www.maji.go.tz**



## HABARI MBEYA

# Mwanafunzi la tatu adaiwa kujinyonga kwa kamba za viatu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWANAFUNZI wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Lungwa iliyopo Kijiji cha Utengule, Kata ya Utengule, Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, Prince Mtivike (9) amefariki dunia baada ya kujinyonga kwa kutumia kamba za viatu pembezoni mwa uwanja wa mpira shuleni hapo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga, aliwaambia waandishi wa habari kwamba tukio hilo lilitokea Mei 2 mwaka huu majira ya saa nane mchana.

**Hili tukio linasikitisha sana lakini pia linatupa somo sisi wazazi kuwa karibu na watoto pamoja na kuwafuatilia ili kujua changamoto wanazopitia ili tuzitatue.**

Kamanda Banga alisema mwanafunzi huyo alijinyonga muda mfupi baada ya kula chakula cha mchana na wanafunzi wenzake shuleni hapo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Msingi Lungwa, Erick Nyongole, aliiambia Nipashe kuwa mwanafunzi huyo alikutwa akiwa amejinyonga pembezoni mwa uwanja wa mpira wa shule hiyo na alipata taarifa kutoka kwa wanafunzi waliokuwa wakicheza pamoja naye.

Baba mkubwa wa mtoto huyo, Alex Mtivike alisema taarifa za kifo cha mtoto wao wamezipata wakiwa Makambako kwa baba mzazi wa mtoto huyo na kueleza kuwa mtoto wao alikuwa na tabia ya kutoroka nyumbani na kukaa mtaani hata kwa siku tatu na kurudi tena nyumbani.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Utengule, Antony Myava na Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Kungwa, Evaristo Mwinami, waliwataka wazazi kuwa karibu na watoto wao ili kujua changamoto zinazowakabili.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Utengule akiwamo Daudi Mlimbila alisema amesikitishwa na tukio la mwanafunzi huyo kujinyonga na kueleza kuwa wataendelea kukaa karibu na watoto ili kujua changamoto zao kabla ya mambo mabaya kutokea.

Alisema: "Hili tukio linasikitisha sana lakini pia linatupa somo sisi wazazi kuwa karibu na watoto pamoja na kuwafuatilia ili kujua changamoto wanazopitia ili tuzitatue."




Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Gilbert Simya (wa pili kulia), akipokea sehemu ya msaada wa vifaa tiba kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya wateja wadogo na wakubwa wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke, vilivyotolewa na benki hiyo, kwa ajili ya kusaidia kuboresha huduma za afya katika Hospitali ya Mpitimbi, mjini Songea, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil.1/- kuhudumia elimu bila malipo shule 120

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe imepokea zaidi ya Sh. bilioni 1.03 kwa ajili ya kuwezesha elimu bila ya malipo katika shule 120 wilayani hapa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Agnetha Mpangile, aliyasema hayo juzi wakati akifungua kikao cha Baraza la Madiwani cha kipindi cha robo ya tatu.

Mpangile alisema halmashauri kupitia mapato ya ndani pia imeendelea kuchangia ujenzi na ukalimishaji wa miundombinu ya elimu katika miradi ya maendeleo.

"Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi machi 2024 ambapo jumla ya miradi mitatu ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi Igagala, Itowo na Matowo na fedha za serikali lakini pia ujenzi wa matundu ya vyoo katika Shule ya Msingi Muhaji na Ilembwe kutumia fedha za wahisani unaendelea," alisema Mpangile.

Hata hivyo, aliwasisitiza madiwani na watendaji kuendelea kuwahamasisha wananchi kuchangia nguvu zao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Nawasisitiza viongozi wa vijiji na kata kusoma mapato na matumizi kwa mujibu wa miongozo iliyopo ili kuweka uwazi wa mapato na matumizi ya fedha zote zilizopokelewa na kutumika kwenye shughuli za maendeleo ikiwamo utambuzi wa nguvu za wananchi," alisema Mpangile.

Awali Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Dk. Peter Nyanja, alisema kati ya halmashauri 184 nchini halmashauri hiyo ni kati ya tano bora ambazo zinatumia mfumo wa Nesti.

"Kwa sababu mafunzo yalifanyika kwa watumishi wote na tumekuwa tukitumia mfumo vizuri, huu mfumo umewekwa kwa nia njema na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya matumizi ya fedha za serikali," alisema Nyanja.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, aliwataka watendaji kusimamia kwa ukaribu miradi ambayo fedha zinatoka serikali kuu sambamba na kuendana na ubora na thamani halisi ya fedha.

Kitta aliwakumbusha viongozi wilayani hapa kwamba wanao wajibu wa kuhakikisha wanatatua kero za wananchi.

Naye Diwani wa Kata ya Wanging'ombe, Geofrey Nyagawa, alisema miradi mingi ya serikali inayopelekwa katika maeneo yao haiwashirikishi wananchi.

## H/Ludewa yapokea bil.1.3/- uchimbaji visima vya maji

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe imepokea Sh. bilioni 1.30 kwa ajili ya uchimbaji visima vya maji pamoja na kukamilisha baadhi ya miradi iliyokwama.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Jeremiah Maduhu aliyasema hayo wakati wa kikao cha jukwaa la wadau wa maji lililofanyika wilayani hapa.

Alisema kwa mujibu wa maelekezo ya serikali kupitia bajeti ya fedha ya mwaka 2024/2025 ilielekeza kuwa Sh. milioni 300 zitatumika katika uchimbaji wa visima na Sh. milioni 700 zitatumika kukamilisha baadhi ya miradi kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva aliwataka watendaji wa kata pamoja na madiwani kuunga mkono ajenda ya Rais Samia Suluhu Hassan iliyolenga kumtua mama ndoo kichwani kwa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji inayotekelezwa katika maeneo yao na kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

Mwanziva alisema kuwa jukwaa hilo limeandaliwa ili kujadili na kuhoji changamoto zilizopo katika miradi mbalimbali na kuweza kuzitatua, ili kuwaondolea wananchi changamoto zinazowasababishia kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya maji.

Alisema: "Pia kuna haja ya kuboresha uunganishaji wa vyombo vya utoaji huduma za maji ngazi ya jamii ili kuwezesha RUWASA kukidhi vigezo vya upataji wa Sh. 50,000 kwa kila mtu ambaye atapata ufikiwaji wa chanzo kilichoboreshwa ikiwamo ujenzi mpya, upanuzi au ukarabati wa skimu ya maji ambapo kwa sasa wilaya yetu bado haijakidhi vigezo vya upataji fedha hiyo," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Wise Mgina, aliwasihi madiwani kuweka usimamizi mzuri ili kuweza kupata fedha hizo kwani vijiji zaidi ya 60 vinapata maji na vinakidhi baadhi ya vigezo.

Alisema: "Viongozi tunapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha tunasimamia uundwaji wa vikundi vilivyokidhi vigezo ikiwamo miradi kutekelezwa kwa ufasaha ili na sisi tuweze kupata hizo fedha ambazo zitatusaidia kuongeza wingi wa miradi ya maji".

# Bei ya petroli Zanzibar yazidi kupaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli visiwani Zanzibar imezidi kupanda na kuuzwa kwa lita moja Sh. 3,182 kwa mwezi huu ikiwa ni tofauti na Aprili iliyokuwa Sh. 3,133.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbaraka Hasan Haji, alitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa bei za mafuta visiwani hapa.

Alisema sababu ya kuongezeka kwa bei ya petroli ni kuongezeka kwa gharama za mafuta katika soko la dunia.

Alisema wakati bei ya petroli ikiwa imepanda bei ya mafuta ya dizeli imeshuka ambapo Aprili iliuzwa Sh. 3,165 na kwa mwezi huu wa Mei inauzwa kwa Sh. 3,146.

Alitaja sababu ya kupunguwa kwa bei ya dizeli na mafuta ya ndege, alisema ni kupunguwa kwa gharama za mafuta katika soko la dunia na kupungua kwa gharama za uingizaji wa mafuta pamoja na mabadiliko ya fedha za kigeni.

Aidha, alisema bei ya mafuta ya ndege kwa mwezi huu yanauzwa Sh. 2,790 na kwa mwezi uliopita yaliuzwa kwa Sh. 2,792 wakati mafuta ya taa bei imesalia kuwa Sh. 3,200.

Alisema ZURA hupanga bei za mafuta kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani, gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es Saalam na Tanga.

Alisema pia gharama za mabadiliko ya fedha za kigeni zinazotumika kununulia mafuta, gharama za usafiri, bima, kodi na tozo za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na reja reja.

Hata hivyo aliwataka wananchi kununua mafuta katika vituo halali vya mafuta na kudai risiti za kieletroniki kila wanaponunua nishati hiyo.

Wakizungumza baada ya kutangazwa kwa bei mpya, baadhi ya wananchi walilamika kuhusu upandaji wa bei na kusema kuwa imeendelea kupanda kwa miezi mitatu mfululizo, huku gharama za maisha nazo kuongezeka.

Ali Bakari ambaye ni dereva pikipiki alisema kupanda kwa nishati hiyo kutaongeza kasi ya mfumuko wa bei wa bidhaa zingine ikiwemo usafiri.

Alisema: "Kutokana na kupanda kwa bei ya petroli gharama zingine nazo zitapanda kwa mfano sisi waendesha bodaboda pahala pakumpeleka mteja kwa shilingi 1,000 sasa itabidi tuongeze gharama lakini unapojaribu kufanya hivyo wateja wanalalamika bila ya kujali bei ya mafuta".

# SMZ, UNESCO kulikarabati jengo la sinema Majestic

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), wanatarajia kulifanyia ukarabati jengo la sinema majestic lililoko katika Hifadhi ya Mji Mkongwe.

Hatua hiyo inalenga kulifanya jengo hilo kuwa kituo kikuu cha utamaduni visiwani hapa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa, aliyasema hayo juzi wakati akifungua warsha ya kujadili mikakati ya ukarabati wa jengo hilo iliyoshirikisha timu ya wataalamu kutoka UNESCO, Japan, Saudi Arabia na Hifadhi ya Mji Mkongwe.

Alisema serikali ina mikakati ya kuhakikisha majengo yote ya Mji Mkongwe yanafanyiwa ukarabati na kurejesha haiba na taswira ya awali.

Leila alisema kukamilika kwa ukarabati huo, kutaongeza vivutio vya utalii nchini na nchi kuendelea kupata watalii wengi zaidi ambao baadhi ya watalii wanaofika visiwani hapa hupenda kujifunza historia.

Aidha, alisema zoezi hilo limelenga kuliboresha jengo hilo lenye historia kubwa na kuendelea kuupa hadhi ya urithi wa dunia.

Alisema mbali ya maonesho ya sinema, ujenzi huo utakapokamilika, litatumika kwa matukio mbalimbali ya kitamaduni, zikiwamo ngoma na filamu za asili, kurekodi kazi za wasanii na kutoa burudani nyingine za kijamii zitakazovutia watalii na wananchi.

Naye Mwakilishi wa UNESCO nchini Tanzania, Michel Toto, alisema shirika hilo litaendelea kuiunga mkono Zanzibar katika mambo mbalimbali yakiwemo ya utamaduni kwa maslahi ya sasa na kizazi kijacho.

Mkurugenzi wa Taasisi ya 'Hifadhi Zanzibar' inayoshirikiana na UNESCO kufanikisha mradi huo, Tolnino Sarav, alisema watahakikisha kazi ya kulifufua jengo hilo inafanyika kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Jengo la sinema Majestic lilijengwa zaidi ya miaka 100 iliyopita, na ukarabati wake unahitaji Dola za Marekani milioni moja hadi kukamilika kwake.

Wadau mbalimbali walioshiriki warsha hiyo, walisifu hatua ya Serikali ya Zanzibar na UNESCO kuja na mradi huo, wakisema una umuhimu mkubwa na jengo hilo ni miongoni mwa vyanzo vya mapato.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohammed Mussa (kulia), akizungumza na Balozi wa Saudia nchini, Yahya Bin Ahmad Okeish (kushoto), Mwakilishi wa UNESCO Tanzania, Michel Toto (wa pili kulia) na Balozi wa Japan nchini, Yusushi Msawa (wa tatu kulia), kabla ya kufungua warsha ya kujadili mradi wa kulitengeneza upya jengo lililokuwa la sinema la Majestic na kuwa kituo kikuu cha utamaduni Zanzibar, mjini Unguja mapema wiki hii. **PICHA: MAELEZO-ZNZ**

# Wataalamu OUT kujifunza teknolojia Ujerumani

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kimetuma wataalamu wake katika Chuo Kikuu cha Bremen Ujerumani ili kujifunza namna ya kutumia teknolojia kwa ufanisi katika ufundishaji.

Hatua hiyo imekuja ikiwa Ujerumani ni miongoni mwa mataifa yaliyopiga hatua kubwa katika maendeleo hasa kwenye sekta ya elimu hususani matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji.

Akizungumzia kuhusu wataalamu hao, Naibu Makamu Mkuu wa OUT, anayeshughulikia taaluma, utafiti na ushauri wa kitaalamu, Profesa Alex Makulilo alisema ziara hiyo imekuwa ni ya muhimu katika ukuaji wa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji.

"Tumekuja kujifunza namna wenzetu wanavyotoa mafunzo kupitia mifumo ya TEHAMA, tumetembelea kituo cha ufundishaji na ujifunzaji mtandao pamoja na kituo cha kutathmini wanafunzi kupitia mtandao katika chuo hiki," alisema Prof. Makulilo.

Alisema ziara hiyo ni zao za ushirikiano uliopo baina ya OUT na Chuo Kikuu cha Bremen, kupitia ushirikiano huo ambapo taasisi hizo hubadilishana uzoefu na kuimarishana zaidi katika maeneo ya ufundishaji, ujifunzaji, utafiti na ushauri wa kitaalamu kwa jamii zao.

"Eneo la kuwafanyia tathmini wanafunzi kupitia mifumo ya TEHAMA ni eneo nyeti ambalo linahitaji umakini mkubwa na OUT tumekuwa tukijifunza kupitia wenzetu ili nasi tuendelee kubuni mifumo bora zaidi katika eneo hili," alisema.

Wanataaluma wengine walioambatana katika ziara hiyo ni pamoja na Prof. Matobola Mihale ambaye ni Mtiva wa Kitivo cha Sayansi, Teknolojia na Taaluma za Mazingira, Dk. Harrieth Mtae ambaye ni Mkurugenzi wa Utafiti, Machapisho na Ubunifu.

Wengine ni Dk. Thimoth Lyanga ambaye ni Matibu Msaidizi wa Mradi wa HEET wa OUT na Dk. Halima Kilungu ambaye ni Mkuu wa Idara ya Jografia, Utalii na Ukarimu.

Akizungumza kwa niaba ya wajumbe wengine Dk. Harrieth Mtae alisema ni jambo la kuishukuru menejimenti ya OUT kuwezesha ziara hiyo.

"Tumechota mengi ambayo tutayatumia kujiimarisha zaidi kutoa taaluma bora kwa wanafunzi kupitia kuimarisha mitaala, kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia na kufanya utafiti kwa manufaa ya nchi yetu," alisema Dk. Mtae.




Mkuu wa Idara ya Huduma za Kadi na Malipo wa Benki ya Exim, Paritosh Babla (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Mgahawa wa Chef's Pride, Salim Mahsen Al Amry, wakionyesha makablasha ya makubaliano ya ushirikiano, baada ya kuzindua tawi la mgahawa huo, jijini Dodoma hivi karibuni. Anayeshuhudia (katikati) ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule. **PICHA: JOHN BADI**

# Daktari ataka wanaorudia uhalifu kupimwa afya akili

**Na Christina Mwakangale**

DAKTARI Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili katika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Godwin Mwisomba, amesema kuna haja ya kupima afya ya akili kwa wanaotenda matukio ya uhalifu na kuyarudia.

Aidha, amesema si jambo la kawaida kwa binadamu kurudia kosa alilofanya na baadhi kupewa adhabu na kutojutia kosa, jambo linaloonyesha kuna uhusiano mkubwa kati ya uhalifu na ugonjwa wa akili.

Bingwa huyo alifafanua hayo jana katika mada iliyohusu uhusiano kati ya magonjwa ya akili na uhalifu kwenye ukurasa wa kijamii mtandaoni Usalama Tv.

"Utafiti ulifanywa katika moja ya magereza huko Afrika Kusini, ulijumuisha watu 280 na hawa watu walikuwa wafungwa jinsi tofauti. Utafiti ulisema magonjwa ya akili yana uhusiano na kurudia kufanya uhalifu.

"Walichogundua zaidi ya theluthi ya watu hao, takribani 82, walikuwa na matatizo mbalimbali kama ya akili. Wengine wana wasiwasi mkubwa, sononа.

"Kuna sababu za kisayansi zinaonyesha wanaorudia uhalifu wana matatizo, changamoto na magonjwa ya akili. Kwa nini? Ukiangalia kuna vitu vitano. Kwanza, ubongo wa gamba la mbele ambao unaweza ukasema umepungua.

"Inapokuja mhemko, yeye anaweza akafanya kitu chochote. Uwezo wake wa kufanya uamuzi kwamba uamuzi huu si sahihi, kwa sasa haupo.

"Anawaza labda kuiba ili akanywe pombe, haoni tatizo. Ila sisi tunalaumu tukio, yeye nafsi yake laumu haipo," alisema Dk. Mwisomba.

Alisema jamii hulaumu tukio lililotendwa bila kufahamu iwapo kuna hitilafu ya ubongo kwa mtenda uhalifu, huku akisema sababu ya pili ya vitendo hivyo ni husababishwa na tatizo la ubongo kushindwa kuhimili hisia.

"Kuna mwitikio wa kihisia, mfano nipite nikamkanyaga mtu na nikahisi na nikamwambia samahani. Lakini utakuta mtu anayefanya uhalifu, hisia zake hazipo au imepungua, hata akipiga mtu ngumi na anamuumiza anaona kawaida," alisema.

Alisema kwa hali ya kawaida, binadamu kupitia sehemu hiyo ya ubongo 'amida', kuna mfumo unaozuia uchokozi, uhalifu na kumpa mtu woga kutenda matendo yaliyo kinyume na jamii anayoishi.

"Kwa watu kama hawa wakiletwa kwa wataalamu kama sisi tunajua namna ya kumpa ushauri na mafunzo. Kwa sababu watu kama hawa hawawezi kuchangamana na jamii kuliko na sheria, utaratibu na yeye hawezi kufuata miongozo, hatambu hana woga."

Bingwa huyo alisema pia katika ubongo kuna mfumo wa zawadi na adhabu, akisema wanaotenda vitendo vya uhalifu na kutojilaumu, mfumo wao upo katika kiwango cha juu.

"Utakuta yeye muda mwingi atakata hali yake ya kujisikia vizuri iwepo muda wote. Hastahimili hali. Mtu wa kawaida kama mfumo wako upo vizuri ukiwa na kiu ukinywa maji, unajisikia vizuri. Lakini hawa wasio na mfumo mzuri hata anywe maji hajisikii vizuri.

"Utakuta mtaani anashindwa kuishi, kila siku yuko polisi. Kuna vitu haviko sawa katika ubongo," alisema.

Alisema kuna hatua za kufanya, akisema watu walio na rekodi ya kurudia vitendo vya uhalifu, wanatakiwa kufanyiwa uchunguzi, ikiwamo ambao wamo katika magereza.

"Kwa wenzetu mtu kama huyu anaweza kupelekwa vitani, lakini kwenye jamii huku atasumbua. Tushirikiane kulishughulikia suala hili pamoja. Tuwatambue watoto wenye kasoro kiakili, ili tuanze mapema kuwafundisha.

"Hawa watu wakiingia kwenye mfumo wa haki jinai, itatumika fedha na rasilimali ya umma katika kuwahudumia watu hawa. Kwa hiyo wenzetu wanatumia utafiti na kusaidia kufanya uamuzi.

"Hii itaipunguzia gharama serikali kwa sababu kuna ambao watapata tiba na wakabadili kabisa tabia. Kuna magonjwa yanaanza utotoni, tunasema huyu mtoto mtukutu, baadae wanakuja kuwa wanajihusisha na uhalifu.

"Tunaweza kuwafikia katika familia na kutoa elimu, wengine ni tabia. Mazingira yanaathiri, labda katika familia wapo wanaotumia dawa za kulevya, watoto wanayabeba, wanaona ukatili kwa baba dhidi ya mama, chanzo mtoto mkatili ni makuzi aliyokulia," alisema Dk. Mwisomba.


NYADHI INVESTMENT Co. LTD

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**M/MWANZO YA KISESA - SHAURI LA JINAI Na. 179/2022**
**INSP. NYAMWAILA......MDAI**
**DHIDI YA**
**YUSUPH MANASE......MDAIWA**

**M/MWANZO YA BUSWELU- SHAURI LA NDOA NA. 01/2023**
**STELLA HUSSEIN......MDAI**
**DHIDI YA**
**HASSAN JUMA......MDAIWA**

**M/MWANZO YA BUSWELU-SHAURI LA TALAKA NA.39/2022**
**TUMAINI PASKALI LUPALIGA......MDAI**
**DHIDI YA**
**PAUL SAGINI KIYUNGA......MDAIWA**

**M/MWANZO MAGU MJINI- SHAURI LA MADAI NA. 98/2023**
**PATRICE THOMAS......MDAI**
**DHIDI YA**
**SAWMELI PAUL......MDAIWA**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO KISESA, MAHAKA YA MWANZO MAGU MJINI, MAHAKAMA YA MWANZO BUSWELU, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA TATU (3), SHAMBA EKARI NANE (8) ZILIZO KIJIJI CHA MWAMABANZA MAGU. MNADA UTAFANYIKA MAHALI MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA 01 ILIYOPO KITONGOJI CHA IGUDIJA „A" KATA YA KISESA WILAYA YA MAGU | IGUDIJA „A"-KISESA | 10/06/2024 SAA4:00 ASUBUHI NA KUENDELA |
| 2 | NYUMBA PLOT NA.104 BLOCK "B" BUSWELU-JIJI LA MWANZA | BULOLA-BUSWELU MWANZA | 21/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA ILIYOPO KAHAMA BUSWELU MKOA WA MWANZA | KAHAMA-BUSWELU - MWANZA | 21/05/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4 | SHAMBA EKARI NANE(8) ZILIZO KIJIJI CHA MWAMABANZA MAGU MKOA WA MWANZA | MWAMABANZA-MAGU | 10/6/2024 SAA4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. KWA MALI INAYOHAMISHIKA, MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI.
2. KWA MALI ISIYOHAMISHIKA, MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**



**KUPOTEA KWA CHETI**



**KIZA HUSSEN JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1489-0046 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KATUBUKA SEKONDARI** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/MAH/RB/438986/2024.**



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**FERDINAND GABO MBOBETSE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 486 AAE** aina ya **TOYOTA CHASER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi.

Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/68217/2024.**



**FORM II**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo BIHARAMULO MJINI**
**Usimamizi wa Mirathi 07...2024**

**Ombi la NEEMA MARTIN MINJA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu ERICK MARTIN MINJA WA RUKARAGATA – BIHARAMULO**

Watu wote wanaodai kuna na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 07/06/2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.





**KUPOTEA KWA CHETI**



**SUZY GALUSY MSEKWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4193/0159 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **HARRISON UWATA GIRL'S SEKONDARY** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MOR/MOR/7218/2024.**

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaionya Israel, yatishia kuinyima silaha

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden, ameionya serikali ya Israel kwamba ikifanya uvamizi kamili wa kijeshi katika mji wa Rafah, nchi yake itasitisha upelekaji na usambazaji wa silaha.

Akizungumza na kituo cha televisheni cha CNN, Rais Joe Biden amesema kwamba Marekani itaacha kusambaza baadhi ya silaha iwapo Israel itaanzisha operesheni ya ardhini katika mji huo uliosongamana watu.

„Ikiwa wataingia Rafah, sitoi silaha ambazo zimetumika kihistoria ambazo zitakabiliana na Rafah,“ alisema wakati wa mahojiano hayo.

Aliendelea kwa kueleza kwamba bado Marekani itaendelea kuhakikisha Israel iko salama wakati wote.

Licha ya upinzani mkali wa Marekani, Israel inaendelea na harakati zake za kufanya uvamizi wa kijeshi katika mji wa Rafah ilioko kusini mwa ukanda wa Gaza.

Mji huo ambao uko mpakani na nchi ya Misri, umekuwa na msongamano wa watu na ndiyo ngome kuu ya mwisho ya kundi la Hamas katika eneo hilo. Hata hivyo, maofisa wa Marekani wameonya kwamba operesheni yoyote ya kijeshi katika mji huo ulioelemewa na idadi kubwa ya watu kutoka maeneo mengine ya Gaza, inaweza kusababisha janga la kibinadamu.

„Hatutasambaza silaha na makombora ya mizinga,“ alisisitiza Rais Biden katika mahojiano hayo yaliyorushwa juzi.

Hata hivyo, hakufafanua kuwa kile kinachoendelea kwa sasa huko Rafah kama operesheni ya chinichini.

„Hawajaingia katika maeneo yenye watu. Walichokifanya ni kufika mpakani, lakini nimeweka wazi kwa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu na baraza la mawaziri la vita, hawatapata uungwaji mkono wetu, kama kweli wataenda katika maeneo yenye watu.“ Aliongeza Rais Biden.

Hata hivyo, kiongozi huyo alikiri kwamba silaha za Marekani ndizo zilitumiwa na Israel kuwaua raia katika Ukanda wa Gaza.

Alipoulizwa kama Israel imevuka, Rais Biden alikataa na kueleza bado haijavuka kiwango hicho.

Wakati huo huo, Balozi wa Israel katika Umoja wa Mataifa, Gilad Erdan, alisema amesikitishwa na kauli hiyo na kueleza kama ya kukatisha tamaa.

„Hii ni kauli ngumu na ya kukatisha tamaa sana kusikia kutoka kwa rais ambaye tumekuwa tukimshukuru tangu mwanzo wa vita,“ alisema Gilad Erdan wakati akizungumza na redio ya umma ya Israel Kan.

„Ikiwa Israel imezuiwa kuingia katika eneo muhimu na la kati kama Rafah ambako kuna maelfu ya magaidi, mateka na viongozi wa Hamas, ni jinsi gani hasa tunapaswa kufikia malengo yetu?“ alihoji kiongozi huyo.

Wakati huo huo, Ofisa wa Umoja wa Mataifa, wa masuala ya wakimbizi wa Kipalestina huko Gaza Scott Anderson, amesema hali inayoendelea ndani ya mji wa Gaza imezidi kutia wasiwasi.

Wiki hii, Israel ilitoa maagizo ya watu kuhama katika maeneo ya mashariki ya Rafah.

Anderson alisema kulikuwa na mapigano upande wa magharibi kuelekea katikati ya Rafah na kusababisha watu 80,000 kuhama makazi yao.


„Labda jambo la kuhuzunisha zaidi, kwa sababu maeneo ya kuingia Kerem Shalom na yamefungwa, tunaanza kukosa mafuta,“ alisema Anderson Aliongeza kwamba ingawa kituo cha mpaka cha Erez ambacho kiko kaskazini bado kiko wazi, kazi zinazoendeshwa ni kidogo kulingana na idadi kubwa ya watu wanaofikia milioni 1.9, ambao wako sehemu ya kusini ya ukanda huo.

„Tunahitaji mipaka kufunguliwa tena ili misaada iendelee kuingia, kwani hivi karibuni tutaona wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa na washirika wetu wa kibinadamu wakianza kukosa chakula hata kuanzia kesho,“ Anderson anasema.

***BBC***



Vifaru vya wanajeshi wa Misri vikipiga kambi karibu na kivuko cha Rafah, baada ya kuwepo kwa mvutano kati ya Misri na Israel karibu na eneo la Philadelphia Corridor. **PICHA: AFP**



## Hofu ya kipindupindu yaikumba Kenya

**NAIROBI, Kenya**

Umoja wa Mataifa umekuwa na wasiwasi kufuatia ugonjwa wa kipindupindu kusambaa nchini Kenya.

Ugonjwa huo ambao umeripotiwa kuripuka katika kaunti ya Tana River, unatokana na mafuriko maji kuikumba nchi hiyo baada ya mvua nyingi kunyesha.

Shirika la Afya Duniani, WHO, lilisema wagonjwa 44 wa kipindupindu wameripotiwa katika kaunti hiyo ambayo ni moja ya maeneo yaliyoathiriwa zaidi na mafuriko.

Mratibu mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini humo, Stephen Jackson, katika mahojiano na kituo cha televisheni cha Citizen, alisema anaamini kuwa kwa ushirikiano kati ya serikali na washirika wa kitaifa na kimataifa, watafanikiwa kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo.

Kulingana na takwimu za hivi karibuni zilizochapishwa na vyombo vya habari vya ndani, mafuriko yamesababisha vifo vya watu 238, huku zaidi ya watu wengine 200,000 wakiachwa bila makazi.

**DW**

# Ugonjwa kifaduro wasambaa Ulaya

**LONDON, Uingereza**

MATAIFA ya Ulaya yameripoti ongezeko la ugonjwa wa kifaduro mwaka 2023 na robo ya kwanza ya mwaka huu na kufanya maambukizi ya ugonjwa kuwa mara 10 zaidi.

Kituo cha kuzuia na kudhibiti magonjwa barani Ulaya, kilisema kuwa wagonjwa 60,000 wa kifaduro wameripotiwa katika bara hilo ndani ya muda wa mwaka jana hadi robo ya kwanza ya mwaka huu.

Ilieleza taarifa hiyo kuwa watu 19 walifariki dunia kutokana na athari ya ugonjwa huo, wakiwamo watoto wachanga 11 na watu wazima wanane.

Nchini Uingereza, wataalamu wa afya wametahadharisha kuwa visa vya ugonjwa huo unaothiri zaidi mapafu huenda vikaongezeka na kufikia kiwango cha juu zaidi kwa muda wa miaka 40.

Ugonjwa wa kifaduro ni maambukizo ya bakteria yanayoathiri mapafu na mfumo wa kupumua na huathiri watu wa rika zote ingawa watoto wachanga na wazee ndio walioko kwenye hatari zaidi.

***DW***

# JOB: KAGERA WALITUPA WAKATI MGUMU JUZI

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya ushindi wa bao 1-0 walioupata juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, beki wa Yanga na nahodha msaidizi wa timu hiyo Dickson Job amesema wapinzani wao waliwapa wakati mgumu kwenye mchezo huo.

Yanga iliwabidi wasubiri mpaka dakika za mwisho kuweza kupata bao lililowahakikishia ushindi kwenye mchezo huo lililofungwa na kiungo Mudathir Yahaya.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Job alisema wapinzani wao walicheza kwa nidhamu kubwa kwenye safu yao ya ulinzi na kuwapa wakati mgumu washambuliaji na viungo wa Yanga kuweza kuwafungua na ili kupata magoli.

"Mchezo ulikuwa mgumu sana, Kagera walicheza kwa nidhamu kubwa, ilitubidi kusubiri wafanye makosa ndipo tupate goli, tunashukuru kwa ushindi huu muhimu," alisema Job.

Aidha, alisema kuwa kwa sasa kila mchezo ni mgumu kwa kuwa kila timu inapambana kutoka kwenye nafasi waliyopo sasa na kupanda juu huku Yanga wakitaka kuutetea ubingwa wao.

"Hatutarajii mchezo mwepesi kwenye michezo iliyobakia, unajua kila timu kwa sasa inapambana kujitoa sehemu ilipo na kupanda juu hivyo hakuna namna tutakuwa na mchezo mwepesi, ni lazima na tupambane ili kufikia lengo la kutetea ubingwa wetu," alisema Job.

Baada ya ushindi huo, mchezo ujao Yanga watakutanana Mtibwa Sugar inayopambana kujiondoa kwenye nafasi ya mwisho katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ushindi wa juzi unaifanya Yanga kufikisha pointi 68 ikiiacha Azam kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi 57 na Simba kwenye nafasi ya tatu ikiwa na pointi 53 (kabla ya mchezo wa jana jioni).

## BONANZA...



Mchezaji wa timu ya Mbozi, Labon Gaitani (aliyevaa jezi nyeupe) akimiliki mpira huku akizongwa na mchezaji wa timu ya Ileje, Gotard Luambano wakati wa mchezo wa bonanza lililoandaliwa na ofisi ya Tanesco mkoa wa Songwe juzi. **PICHA FRIDAY SIMBAYA**

# Mashujaa FC yataja siri iliyowabeba kuiua KMC

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya KMC, Kocha Mkuu wa Mashujaa FC, Abdallah Mohamed 'Bares' amesema siri ya kuvuna pointi tatu muhimu katika mchezo huo ni utulivu waliokuwa nao washambuliaji wake.

Ushindi huo umeifanya Mashujaa kufikisha pointi 26 na kusogea hadi nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bares alisema waliwaandaa wachezaji wake kucheza kwa umakini na kutokuwa na hofu ili kupata ushindi na kuanza kujiondoa katika janga la kushuka daraja.

Bares alisema pia uamuzi wa kubadilisha kikosi umesaidia kuwapa nguvu ya kutawala mechi hiyo na hatimaye kufikia malengo.

Kocha huyo alisema mechi hiyo ilikuwa muhimu sana kwao hasa baada ya kushindwa kuondoka na pointi katika mchezo wao uliopita dhidi ya Yanga ambao walifungwa bao 1-0.

"Utulivu waliokuwa nao wachezaji wetu umetusaidia kupata ushindi, lakini mabadiliko yaliyoonekana jana (juzi) yameifanya timu kuwa na kasi, tumetumia wachezaji wengi vijana ambao wana nguvu na wametupa kile tulichokihitaji," alisema Bares.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Reliants Lusajo, alisema wachezaji waliingia uwanjani kwa lengo moja la kupambana na kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

"Ilikuwa ni mechi muhimu sana kwetu, tulisema tunatakiwa kupambana, tusicheze kwa hofu na tusahau matokeo ya michezo ya nyuma," alisema Lusajo.

Aliongeza ushindi huo utawaongezea morali ya kupambana katika mechi zinazofuata na hatimaye kuibakiza timu yao kwenye ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

Mashujaa FC sasa itasafiri kuelekea Tabora kuwafuata Tabora United kwa ajili ya mchezo utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani humo.

## Viungo Dodoma Jiji waitisha TZ Prisons

**Na Somoe Ng'itu**

LIGI Kuu Bara inatarajia kuendelea leo wakati Dodoma Jiji FC inatarajia kuwakaribisha 'Maafande' wa Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Lyogope, amesema timu yake imejiandaa vizuri na anaamini watashuka dimbani kwa lengo moja la kuzibakisha pointi tatu muhimu nyumbani.

Lyogope alisema wanaipa umuhimu mkubwa mechi hiyo kwa sababu wanakutana na timu yenye wachezaji wazoefu na waliokaa pamoja kwa muda mrefu.

"Tunajua mechi itakuwa ngumu kwa sababu tunakutana na timu yenye ubora, tutaingia kwa tahadhari kwa sababu tunaipa umuhimu mkubwa mchezo huo, tunajua hatuko katika nafasi nzuri katika msimamo," alisema Lyogope.

Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Hamad Ally, aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mechi hiyo ambayo itakuwa na ushindani kutoka katika pande zote mbili. Ally alisema wanahitaji kupata matokeo mazuri ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi ambao mpaka sasa huwezi kufahamu nani anaweza kushuka daraja.

"Tumefanya maandalizi mazuri kwa siku ya jana (juzi) na leo (jana), wachezaji wako vizuri isipokuwa mmoja ndio majeruhi, tunajua tunaenda katika mchezo mgumu, Dodoma Jiji inawachezaji wazuri sana katika eneo la kiungo, wanajua kutengeneza nafasi na kumiliki mpira," alisema Ally.

## Kocha Kundemba FC ashusha lawama kwa mabeki wake

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa Kundemba FC, Mohmed Seif 'King', amesema makosa katika safu ya ulinzi ya timu hiyo ndio inayopelekea kutopata matokeo mazuri katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar.

Kundemba FC juzi ilijikuta ikipokea kipigo cha mabao 3-2 kutoka kwa Mafunzo FC kikiwa kipigo cha tatu mfululizo.

Timu hiyo bado ipo katika mstari wa hatari wa kushuka daraja na ikiwa imebakisha michezo saba tu kumaliza msimu huu wa Ligi Kuu.

Akizungumza na Gazeti hili kocha huyo alisema timu yake inacheza vizuri na kwa hamasa kubwa lakini inashindwa kupata matokeo ya alama tatu kutokana na safu ya ulinzi kushindwa kulinda magoli wanayoyapata lakini pia kuruhusu magoli mepesi.

Alisema katika safari yao ya kuinusuru timu hiyo kushuka daraja anatakiwa kuyafanyia kazi makosa hayo katika safu ya ulinzi ambayo ameyaona katika michezo miwili mfululizo.

## ZISIKUPITE

### NUNEZ NA BARCELONA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Uruguay, Darwin Nunez, ameibuka kama lengo kuu la kushtukiza kwa Barcelona, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 akionekana kama mbadala wa mshambuliaji wa Poland Robert Lewandowski mwenye miaka 35.**(Sun)**

### ...ACHOCHEA MOTO

DAREIN Nunez amechochea uvumi wa kuondoka Liverpool majira ya joto kwa kufuta picha zote za wakati wake Anfield kwenye ukurasa wake wa Instagram. **(90min)**

### SANCHO HAITAKI UNITED

MSHAMBULIAJI wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 24, hataki kurejea Manchester United mwishoni mwa muda wake wa mkopo katoka Borussia Dortmund.**(Talksport)**

### CHELSEA YAMKOMALIA SUDAKOV

CHELSEA imezidisha juhudi zao za kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Shakhtar Donetsk raia wa Ukraine mwenye thamani ya pauni milioni 65 Georgiy Sudakov mwenye umri wa miaka 21, ambaye anafuatiliwa na Arsenal, Manchester City na Liverpool.**(Mail)**

### OSIMHEN NAE KWENYE RADA

CHELSEA pia wanataka kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa kwa zaidi ya pauni milioni 100.**(Sky Italia)**

### OBLAK AWINDWA CHELSEA

GOLIKIPA wa Atletico Madrid na Slovenia, Jan Oblak mwenye umri wa miaka 31, ni mchezaji mwingine ambaye yuko kwenye rada ya Chelsea msimu huu wa joto, huku klabu yake ya Hispania ikitaka kuchangisha fedha kwa ajili ya kujenga upya kikosi. **(Fichajes)**

### IVAN TONEY AGOMBEWA

KLABU ya West Ham United na Tottenham Hotspur ndio zilizo mstari wa mbele kuwania kumsajili mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 28, msimu huu wa joto, huku timu zote zikipanga kutoa takriban pauni mil. 50. **(Football Transfers)**

### GYOKERES NJIA PANDA LISBON

MSHAMBULIAJI wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 25, amekataa kutoa hakikisho la kubakia katika klabu ya Sporting Lisbon huku Arsenal ikimtaka. **(Standard)**

### UNITED KUMPIGA BEI CASEMIRO

KLABU ya Manchester United inajaribu kutafuta mnunuzi wa kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 32 msimu huu wa joto ili kujaribu kupunguza mzigo wa mishahara. **(TEAMtalk)**

### SLOT KUIBOMOA FEYENOORD

ARNE Slot, ambaye anatarajiwa kuchukua nafasi ya kocha anayeondoka Jurgen Klopp kule Liverpool, anaweza kurejea Feyenoord ili kuwasajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Mats Wieffer mwenye umri wa miaka, 24, na mlinzi wa Uholanzi Lutsharel Geertruida mwenye miaka 23.**(Football Insider)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BEKI ADARABIOYO AWANIWA MAN U

Nyota huyo anamaliza mkataba wake Fulham mwisho wa msimu na anaweza...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumsajili beki wa Fulham, Tosin Adarabioyo msimu huu wa joto, vyanzo vimeiambia ESPN.

Adarabioyo anamaliza mkataba wake pale Craven Cottage mwishoni mwa msimu huu na anaweza kuhamia Old Trafford kwa uhamisho wa bure.

Newcastle United, Chelsea na Tottenham Hotspur pia zimeonyesha nia ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye amecheza mechi 20 za Ligi Kuu msimu huu na kufunga mara mbili.

Mchezaji huyo wa zamani wa timu ya taifa ya England alijiunga na Fulham kutoka Manchester City mwaka wa 2020.

Pia amekuwa na muda wa mkopo katika klabu za West Bromwich Albion na Blackburn.

Adarabioyo alitia saini kurefusha mkataba na Fulham Januari 2023, lakini anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo mkataba wake utakapokamilika Juni.

United wanatazamia kusajili beki wa kati msimu huu wa majira ya joto kama sehemu ya marekebisho ya kikosi katika dirisha la kwanza la usajili linalosimamiwa na timu mpya ya uongozi wa klabu hiyo iliyoteuliwa na mmiliki mwenza Sir Jim Ratcliffe.

Mkurugenzi mpya wa ufundi Jason Wilcox anamfahamu Adarabioyo vyema kutoka wakati walipokuwa pamoja Manchester City.

Wilcox alifanya kazi katika akademi ya City kabla ya kujiunga na Southampton kama mkurugenzi wa soka.

Kuna mashaka juu ya mustakabali wa mabeki kadhaa wa kati waliopo United, wakiwamo Raphaël Varane, Harry Maguire, Victor Lindelöf na Jonny Evans.

# JOSELU: FURAHA YANGU HAIPIMIKI KUFUZU FAINALI

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Joselu amesema furaha yake haipimiki baada ya kushuhudia timu yake ikitinga hatua ya fainali baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Bayern Munich juzi usiku huku akifunga mabao yote.

Alphonso Davies aliyetokea benchi alikuwa ameiweka Bayern mbele dakika ya 68 ya mchezo wa marudiano wa nusu fainali Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Hata hivyo, Joselu alisawazisha dakika ya 88 na kufunga tena dakika ya 91 akiunganisha krosi ya Antonio Rüdiger na kuifanya Madrid kufuzu fainali kwenye Uwanja wa Wembley jijini London mnamo Juni 1, ambapo watamenyana na Borussia Dortmund.

„Sijui kuhusu kuwa shujaa, lakini nina furaha sana," alisema Joselu akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.

„Unaweza kufikiria! Ilikuwa ya ajabu, ya kuvutia. Timu hii haikati tamaa. Kupambana hadi mwisho ni katika damu yake."

Madrid sasa wamefuzu kwa fainali sita za Ligi ya Mabingwa ndani ya miaka 11, baada ya kushinda ubingwa huo mwaka 2014, 2016, 2017, 2018 na 2022.

Watakuwa na nafasi ya kubeba mataji mawili baada ya kuchukua LaLiga msimu huu.

„Unaota kila wakati kuhusu aina hii ya uchezaji," alisema Joselu.

„Bao la kwanza lilikuwa ni kuwa mwerevu, na kuwa tayari. Walikuwa wamechoka ... Hata ndoto zangu nzuri sio nzuri kama kilichotokea leo (juzi)."

„Imetokea tena," alisema kocha Carlo Ancelotti.

„Ni jambo lisiloelezeka, na limetokea tena, likiwa na mazingira mazuri, na wachezaji ambao hawakuacha kuamini.

„Ulikuwa mchezo mgumu, tulipata nafasi, tulikuwa na udhibiti, kisha tukawa na nguvu ya kutopoteza vichwa vyetu. Lazima niwashukuru mashabiki, klabu na zaidi ya wachezaji wote ambao wamekuwa na msimu ambao hakuna mtu aliyetarajia.

„Sikutarajia kikosi hiki kufanya kile ambacho wamefanya pia. Kufika fainali ni mafanikio, halafu lolote litakalotokea, hutokea."

Joselu mwenye umri wa miaka 34, alijiunga na Madrid kwa mkopo kutoka Espanyol msimu uliopita wa joto na amefunga mara tisa kwenye LaLiga na mara tano kwenye Ligi ya Mabingwa.





## Enrique kubaki PSG

**PARIS, Ufaransa**

LUIS Enrique atasalia kama kocha wa PSG msimu ujao, vyanzo viliiambia ESPN licha ya klabu hiyo kutolewa katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mbele ya Borussia Dortmund Jumanne.

PSG iliwafuta kazi makocha siku za nyuma baada ya kushindwa katika Ligi ya Mabingwa, lakini vyanzo vimeiambia ESPN klabu hiyo inafurahishwa na kazi ya Enrique na inaamini kuwa anaweza kuipeleka klabu mbali zaidi.

Kocha huyo wa Hispania, ambaye alifikisha umri wa miaka 54 Jumatano, alisaini mkataba wa miaka miwili alipojiunga na PSG msimu uliopita wa joto na anaweza kuanza mazungumzo ya kuongeza muda hivi karibuni.

Enrique amekuwa kipenzi cha mashabiki msimu huu, wakiwamo wafuasi wakali wa klabu hiyo ambao huimba jina lake katika kila mchezo.

Kazi ya kuiongoza PSG kutwaa taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya itakuwa ngumu zaidi msimu ujao iwapo Kylian Mbappé atatimiza uamuzi wake wa kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa mkataba wake msimu huu wa joto na kujiunga na Real Madrid.

Hata hivyo, Enrique hajakwepa kuachana na wachezaji nyota katika klabu ya PSG alichukua uamuzi wa kijasiri kuwaruhusu Neymar na Marco Veratti kuondoka Parc des Princes msimu uliopita wa joto na badala yake amejikita katika kuweka ari ya timu na utambulisho wake.

Licha ya kwamba mbio zao za Ligi ya Mabingwa Ulaya zimefikia kikomo, PSG bado wanaweza kuongeza mataji yao msimu huu kwenye fainali ya Kombe la Ufaransa Mei 25 ambapo watamenyana na Lyon.

PSG tayari wamenyanyua Ligue 1 msimu huu katika msimu wa kwanza wa Enrique kama kocha, pamoja na Kombe la Super Cup la Ufaransa.

## Klabu mbili zamtaka Greenwood

**LONDON, England**

KLABU mbili za Ligi Kuu England zimeulizia kuhusu fowadi wa Manchester United, Mason Greenwood, kulingana na ripoti mpya, lakini kuhamia nje ya nchi kuna uwezekano mkubwa zaidi kwa wakati huu.

Greenwood ametumia msimu huu kwa mkopo Getafe baada ya United hatimaye kutambua „ugumu wa yeye kuanza tena kazi yake" katika klabu hiyo, na kuamua „itakuwa sahihi zaidi kwake kufanya hivyo nje ya Old Trafford".

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amefunga mabao kumi katika mechi 31.

Man United wanapendelea zaidi kumuuza, ingawa kuanzishwa kwa chaguo la nyongeza la miezi 12 katika mkataba wake ili kumzuia Greenwood kuwa mchezaji huru mnamo 2025 na kupanga mkopo wa pili haijakataliwa ikiwa ofa inayofaa itashindwa kutekelezwa.

Gazeti la Telegraph liliandika kwamba United wanamthaminisha Greenwood kwa ada sawa na ile iliyomchukua Cole Palmer kwenda Chelsea msimu uliopita wa majira ya joto kati ya pauni milioni 40 hadi 45 na kwamba klabu mbili za Ligi kuu England ambazo hazikutajwa zimeuliza kuhusu yeye.

Hata hivyo, inapendekezwa kuwa fowadi huyo ‚bado ana uwezekano mkubwa' wa kucheza nje ya England.

Inasemekana kuna uangalizi wa karibu kutoka kwa Atletico Madrid, huku Barcelona wakimtaka pia, lakini hawana fedha na Real Madrid hawakuona uwezekano wa kumfuatilia.

Vilabu ambavyo havijatajwa nchini Ujerumani pia vinahusishwa, wakati kuna nia kutoka kwa pande za Italia ambazo zinaweza kujumuisha Juventus na Lazio kufuatia uvumi wa hivi majuzi.

Baada ya uchunguzi wa ndani wakati mashtaka ya jinai yalipotupiliwa mbali huku mashahidi muhimu wakiondolewa na ushahidi mpya kufichuka, United awali ilitarajiwa kujaribu kumjumuisha Greenwood kwenye kikosi chao hadi pale msukosuko ulipotokea.

Sir Jim Ratcliffe baadaye aliacha mlango wazi kwa mchezaji huyo ambaye bado ana mustakabali kwenye klabu mara tu alipofika kama mmiliki mwenza wa wachache kwa kupendekeza kwamba uamuzi mpya ungetolewa.

Walakini, bilionea huyo alipuuza maoni yake kwa kusema kwamba mashabiki „kuridhika nayo" lazima iwe sababu.

HABARI MICHEZO

# MZINZIRO 'AIVULIA KOFIA' YANGA AWAPONGEZA WACHEZAJI WAKE

Na Faustine Feliciane

KOCHA wa Kagera Sugar, Fred Felix ‚Minziro' amesema ubora wa wachezaji wa Yanga ndio uliamua mechi ya juzi ambayo walipoteza kwa bao 1-0.

Minziro alisema Yanga wana wachezaji wenye ubora mkubwa ambao wanaweza wakabadilisha matokeo muda wowote ndio sababu pamoja na timu yake kucheza vizuri na kuwabana wapinzani wao bado walitumia vyema kosa moja walililofanya wachezaji wake.

„Ubora wa wachezaji wa Yanga uliamua mechi, tulicheza vizuri muda mwingi wa mchezo lakini kosa moja tulilolifanya walituadhibu, kwangu mimi naona ni ubora wa wachezaji tu umeamua mechi, tulicheza vizuri na nawapongeza wachezaji wangu kwa kucheza vizuri,“ alisema Minziro.

Alisema dakika za mwisho kulikuwa na umakini mdogo kwa safu yake ya ulinzi na kupelekea yanga kutumia makosa hayo kupata goli lililofungwa na kiungo Mudathir Yahaya.

"Mabeki walichelewa kufika kwenye nafasi kwa haraka na kumpa nafasi Mudhathir kutuadhibu, hata hivyo mchezo huu umepita tunajipanga kwa ajili ya mchezo mwingine wa mbele yetu,“ alisema Minziro.

Alisema wanapaswa kupambana katika michezo iliyobakia ili kuweza kujiondoa kwenye nafasi waliyopo sasa na kupanda juu kabla ya kujua hatima yao mwishoni mwa ligi.

Kagera Sugar inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC ikiwa na pointi 30 baada ya kucheza michezo 26, hata hivyo imezizidi michezo miwili timu mbili za chini yake, JKT Tanzania na Singida Big Stars ambazo zote zina pointi 29.



Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahaya (katikati) akishangilia goli pekee aliloifungia timu yake dhidi ya Kagera Sugar juzi katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara juzi kwenye uwanja wa Azam Complex, Yanga ilishinda bao 1-0, kushoto ni Joseph Guede na nyuma ni Maxi Nzengeli. **PICHA:BINZUBEIRY**

# Maxime aigawanya Ligi Kuu 'mara tatu'

Na Somoe Ng'itu

WAKATI Kocha Mkuu wa Ihefu (Singida Black Stars), Mecky Maxime, akisema mechi zote zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara ni fainali, amesema kuna 'vita' za aina tatu katika ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

Ligi Kuu Tanzania Bara imeingia katika raundi ya 26, zimebakia raundi nne na inatarajiwa kumalizika rasmi Mei 28, mwaka huu kwa timu zote 16 kushuka dimbani.

Maxime aliliambia gazeti hili hakuna mechi rahisi iliyobakia katika ligi hiyo kwa sababu kila timu inapambana kusaka ushindi.

Kocha huyo alisema timu zote zinaendelea kufanya maboresho katika vikosi vyao kwa sababu wanataka kuvuna alama muhimu ambazo zitawasaidia kufikia malengo.

" Ligi imefikia mahali ambazo kila mechi ni sawa na fainali, kuna vita ya kuwania ubingwa, vita ya kujiweka mahali salama na vita ya kubakia kwenye ligi, kwa maana hiyo hakutakuwa na mechi rahisi, kila mmoja anashuka dimbani na malengo yake," Maxime, nahodha huyo wa zamani wa Taifa Stars alisema.

## Gamondi awapa neno wachezaji

INATOKA UK. 24

hisi kwa timu zilizo kwenye eneo la hatari kwenye msimamo kwa sababu wanahitaji kujiondoa huko, kufanya hivyo wanapambana sana hasa wanapocheza na timu kubwa kama Yanga.

Alisema ana hofu na michezo ya ugenini kutokana na aina ya viwanja wanavyoenda kuchezea pamoja na umuhimu wa pointi tatu kwa wapinzani wao.

„Tuna michezo ya ugenini, pamoja na upinzani kutoka kwa wenyeji wetu, lakini pia viwanja vimekuwa changamoto kwetu, hivyo lazima tuhakikishe tunacheza kwa malengo na kujituma zaidi, baada ya mchezo na Kagera nimewaambia wachezaji wangu nini nataka kwenye michezo hiyo iliyobaki,“ alisema Gamondi.

Yanga wanaongoza wakiwa na pointi 68 huku wakibakiza michezo minne kabla ya ligi kumalizika ambapo watakuwa na michezo miwili ugenini wakianza na Mtibwa Mei 13.

Baada ya mchezo huo watakuwa na kibarua kingine cha mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Ihefu FC utakaochezwa kati ya Mei 17 au 18.

Mei 22 watakuwa ugenini dhidi ya Dodoma Jiji FC baada ya hapo watarudi nyumbani kucheza na Tanzania Prisons na baadaye kumalizana na Tabora United.

## Milioni 300/- Kibu Simba

INATOKA UK. 24

alikihitaji.

Winga huyo ambaye hucheza kama mshambuliaji wa kati, alijiunga na Simba 2021, akitokea Mbeya City na anamaliza mkataba wake wa awali mwishoni mwa msimu huu.

Alipoulizwa juu ya taarifa hiyo, Meneja Habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema Simba wapomakini kwenye masuala yao ya usajili na hakuna mchezaji wanayemuhitaji ataondoka Simba na kujiunga na klabu nyingine ya hapa nyumbani.

Alisema uongozi utatoa taarifa kama kuna jambo lolote limefanyika kuhusiana na usajili.

Wakati huo huo, Simba ipo kwenye mpango wa kumsajili golikipa wa kimataifa wa Cameroon, Joseph Fabrice Ondoa ambaye anacheza soka lake nchini Ufaransa iwapo kipa wake, Ayoub Lakred ataamua kuondoka.

Kipa huyo mwenye miaka 28 makuzi yake ya soka aliyapata kwenye chuo cha soka cha Samuel Eto'o, kwa sasa anaidakia klabu ya Nimes Olympique ya Ufaransa inayoshiriki ligi ya National, ambayo ni Ligi Daraja la Pili nchini humo.

Ahmed akizungumzia hilo pia alisema, „kwa sasa tetesi za usajili ndiyo kipindi chake, hivyo siwezi kuzuia kile kinachosemwa, lakini taarifa kamili za klabu kuhusu usajili na wachezaji tunaowaongezea mikataba na hata wale tutakaowaacha zitatolewa kwa utaratibu maalum baada ya Ligi Kuu kumalizika,“ alisema Ahmed.

# Michezo

Ijumaa Mei 10, 2024

Nipashe


**Joselu: Furaha yangu haipimiki kufuzu fainali**

UKURASA 22



# MILIONI 300/- ZAMBAKISHA KIBU SIMBA

## ●●● Aipiga chini ofa ya Yanga, pande mbili zakubaliana mkataba wa miaka miwili na mshahara wa...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mvutano mkubwa kati ya klabu ya Simba na mshambuliaji wake Kibu Denis juu ya kusaini mkataba mpya, taarifa zinasema kuwa pande hizo mbili hatimaye zimefikia makubaliano na nyota huyo atasalia klabuni hapo kwa misimu miwili zaidi.

Taarifa ya uhakika zinasema Kibu kupitia kwa wawakilishi wake amekubali kusaini mkataba mpya wa miaka miwili wenye thamini ya shilingi milioni 300 (sawa na milioni 150 kwa kila mwaka).

Mmoja wa watu wa karibu wa mchezaji huyo aliiambia Nipashe jana kuwa licha ya Yanga kuwasilisha ofa yao, Kibu ameamua kusalia Msimbazi baada ya kukubaliana dau na nyongeza kubwa ya mshahara wake.

„Nikwambie tu kuwa Kibu ameamua kusalia Simba mpaka Juni 2026, amesalia kwa ada ya uhamisho Sh. milioni 300, amepewa Sh.milioni 150 kwanza na nusu nyingine atamaliziwa," alisema mtoa taarifa huyo.

Alisema ni kweli klabu ya Yanga ilikuwa imemwekea Kibu dau la Sh. milioni 350 na ilikuwa tayari kutoa zaidi ya hiyo, lakini ongezeko hilo limekuja wakati tayari mchezaji huyo ameshasaini mkataba wa awali na Simba.

„Siyo uongo, kuna watu wanasema sijui meneja wake alikuwa akitaja Yanga kumtaka ili kumpandisha thamani, si kweli, jamaa kweli walikuwa wanamhitaji na ilibaki kidogo tu.

„Kilichosababisha ishindikane ni kwamba, Yanga ilitoa ofa ya Sh. milioni 350, lakini ongezeko hilo lilionekana ni dogo kwa mchezaji na kuona ni bora abaki kwenye klabu ambayo ameizoea.

Baadaye Yanga ikaja na ofa nyingine nono zaidi ya hiyo, lakini kwa bahati mbaya ilikuwa imeshachelewa kwani mchezaji alikuwa ameshasaini mkataba wa awali na klabu yake ya zamani, hapo ndipo mchezo ulipoishia, kama ofa ya pili ingeletwa mapema kabla hajasaini Simba saa hizi tungekuwa tunaongea mengine, jamaa amebaki Simba," alisema mtu huyo wa karibu na Kibu.

Alisema, katika mkataba wake huo mpya, mshahara wake umepanda kutoka Shilingi milioni nane mpaka shilingi milioni 15 kwa mwezi kiasi ambacho Kibu

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji wa Real Madrid, Vinicius Junior, akimtoka mchezaji wa Bayern Munich katika mchezo wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi usiku kwenye uwanja wa Santiago Bernabeu nchini Hispania, Madrid ilishinda mabao 2-1 na hivyo kutinga fainali ya michuano hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# Gamondi awapa neno wachezaji wake

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

BAADA ya ushindi wa juzi wa dakika za mwisho wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi ametoa neno kwa wachezaji wake akiwataka kuongeza umakini na kutodharau mpinzani wao kwenye michezo iliyobakia kuhitimisha Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Gamondi amekiri kuwa kwa sasa kila mchezo ni mgumu kutokana na umuhimu wa pointi tatu kwa kila timu hivyo wanapaswa kuwa makini katika kila mchezo hasa ile watakayocheza ugenini.

Yanga imebakisha michezo minne kumaliza ligi ambapo michezo miwili watacheza ugenini dhidi ya Mtibwa Sugar na Dodoma United na michezo miwili watacheza nyumbani dhidi ya Tabora United na Tanzania Prisons.

Akizungumza jana, Gamondi alisema michezo hiyo iliyobakia ni muhimu sana kwao lakini haitakuwa michezo rahisi kwao kutokana na wapinzani wao kuhitaji pointi tatu ili kujinasua katika nafasi walizopo sasa kwenye msimamo.

„Tunatakiwa kuongeza umakini zaidi, mchezo dhidi ya Kagera Sugar umetupa picha ya ugumu wa michezo ya mwishoni mwa ligi, kila timu inapambana kujinasua katika nafasi walizopo sasa hivi lazima wachezaji wangu wawe makini na kupambana muda wote wa mchezo ili kufikia malengo ya kutetea ubingwa wetu," alisema Gamondi na kuongeza,

„Ni ngumu sana kupata pointi tatu kira-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >